# SILAHA ZA MAHUBIRI

Mwandishi - Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania ©

nakala 5000 Chapa ya mara ya kwanza 1999
nakala 5000, Nairobi Kenya Chapa ya mara ya pili 2000
Chapa ya mara ya tatu 2001 nakala 5000
Chapa ya mara ya nne 2002 nakala 5000

Kimeenezwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
P. O. Box 376
Dar es Salaam -Tanzania
Tel: 2110473 . Fax: 2121744

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ ۝

# UTANGULIZI

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu siku hizi watu wanapenda kujua na kujiunga na Dini ya Kiislamu. Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ni Jumuiya ya Mwenyezi Mungu; na hivyo ni jukumu la kila Mwanajumuiya kutangaza na kufundisha neno la Mwenyezi Mungu ili watu wapate kujiunga na Jumuiya kwa wingi.

Kitabu hiki kimetayarishwa kwa ajili ya Daiyan ila llah ili kuwahakikishia wengine ukweli na uzuri wa dini ya Kiislamu. Wahubiri wajaribu kukielewa na kukitumia vizuri kijitabu hiki. Nina yakini kwamba mhubiri ambaye atajua kutumia maandishi haya; kwa msaada wa Mwenyezi Mungu ushindi utabusu miguu yake.

Tumtangulize na tumtegemee Allah Mola wetu atusaidie kutangaza neno Lake na Awaonyeshe watu dalili zilizo waziwazi za ukweli wake.

Muzaffar Ahmad Durrani
Amir na Mbashiri Mkuu.
Ijumaa, Sept 10, 1999. Friday the 10th.

# KIFO CHA NABII ISA A.S.

وَكُنتُ عَلَيۡهِمۡ شَهِيۡدًا مَّادُمۡتُ فِيۡهِمۡ فَلَمَّا تَوَفَّيۡتَنِىۡ كُنتَ
اَنۡتَ الرَّقِيۡبَ عَلَيۡهِمۡ وَاَنۡتَ عَلٰى كُلِّ شَىۡءٍ شَهِيۡدٌ ۝

... na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa kati yao, lakini Uliponifisha Wewe Ukawa Mchungaji juu yao, na Wewe ni Shahidi juu ya kila kitu. (5:118).

**(i) Maana ya neno *Tawaffa* ni kifo.**

Neno hili linapotumika kumhusu mwanadamu; Mwenyezi Mungu akiwa mtendaji *(Faailu)* na mwanadamu akiwa mtendwaji *(Mafuulu)* na kisha neno hilo *tawaffa* lisifuatiwe na *karina* (neno la kuliongezea maana zaidi kama vile 'usiku' au 'kulala'), basi siku zote linamaanisha kufa tu.

## TAMBIO

Mtu yeyote atakayeleta mfano ulio kinyume na kanuni hii atapata zawadi ya TSh. 100,000/-.

## Neno tawaffa katika Qur'an.

4:16; (e) 4:98; (f) (a) 5:118; 22:235; (b) 2:241; (c) 3:194; (d) 7:127; (h) 13:41; (i)10:47; 13:41; (j) 12:102; (k) 16:29; 6:62; (g) 40:78; (l) 16:71; (m) 22:6; (n) 32:12; (o) 39:43; (p) 40:68; (q) (r) 47:28; (s) 8:51; (t) 10:105. (u) 2:235.

Tawaffa yenye karina 39:43; 6:61.

(ii) فَاَقُوۡلُ كَمَا قَلَ الۡعَبۡدُالصَّالِحُ عِيۡسَى بۡنُ مرۡيَمَ وَكُنۡتُ عَلَيۡهِمۡ شَهِيۡدًا مَّادُمۡتُ فِيۡهِمۡ فَلَمَّا تَوَفَّيۡتَنِىۡ كُنۡتَ اَنۡتَ الرَّقِيۡبَ عَلَيۡهِمۡ ۝

Mtume Muhammad s.a.w. alisema na yeye atajibu kama alivyojibu Nabii Isa a.s. juu ya masahaba zake watakaopelekwa motoni. *(Sahihi Bukhari, Kitab Tafsir).* Tafsiri ya Aya ya 118 ya Sura ya 5.

(iii) مُتَوَفِّيۡكَ اَى مُمِيۡتُكَ

*Mutawaffika,* maana yake nitakufisha. (Bukhari Kitabu cha Tafsiri, tafsiri ya Aya ya 118 ya sura ya 5).

2. وَمَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوۡلٌ قَدۡ خَلَتۡ مِنۡ قَبۡلِهِ الرُّسُلُ اَفَائِنۡ مَّاتَ اَوۡ قُتِلَ انۡقَلَبۡتُمۡ عَلٰٓى اَعۡقَابِكُمۡ ۝

Na siye Muhammad ila yu Mtume. Bila shaka wamekwisha fariki kabla yake Mitume wote. Je, akifa au akiuawa mtarudi nyuma kwa visigino vyenu? Na Atakayerudi nyuma kwa visigino vyake hatamdhuru Mwenyezi Mungu cho chote; Na

Mwenyezi Mungu bila shaka Atawalipa wanaoshukuru. (3:145).

مَاالْمَسِيْحُ ابْنُ مَرْيَمَ اِلَّا رَسُوْلٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ وَاُمُّهٗ صِدِّيْقَةٌ كَانَا يَاْكُلٰنِ الطَّعَامَ اُنْظُرْ كَيْفَ نُبَيِّنُ لَهُمُ الْاٰيٰتِ ثُمَّ انْظُرْ اَنّٰى يُؤْفَكُوْنَ ۝

Masihi bin Mariam siye ila ni Mtume tu; bila shaka Mitume wote wamekwisha fariki kabla yake; na mama yake ni mwanamke mkweli; wote wawili walikuwa wakila chakula. Tazama jinsi Tunavyowabainishia Aya, kisha tazama wanageuzwa wapi? (5:76).

4. وَمَا جَعَلْنٰهُمْ جَسَدًا لَّا يَاْكُلُوْنَ الطَّعَامَ وَمَا كَانُوْا خٰلِدِيْنَ ۝

Wala Hatukuwajaalia (manabii) miili isiyokula chakula, wala hawakuwa wenye kukaa (milele). (21:9)

5. وَمَآ اَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِيْنَ اِلَّآ اِنَّهُمْ لَيَاْكُلُوْنَ الطَّعَامَ ۝

Na Hatukupeleka kabla yako Mitume ila bila shaka walikuwa wakila chakula. (25:21).

6. اِذْ قَالَ اللّٰهُ يٰعِيْسٰىٓ اِنِّىْ مُتَوَفِّيْكَ وَرَافِعُكَ اِلَيَّ

(Kumbukeni) Mwenyezi Mungu aliposema: Ewe Isa, kwa yakini Mimi Nitakufisha na Nitakuinua Kwangu, .... (3:56).

<u>**Neno *Raf'a***</u> linapotumika kumhusu mwanadamu, yeye akiwa ni mtendwaji (Maf'uulu) na Mwenyezi Mungu akiwa mtendaji (Faailu) siku zote linamaanisha kuinua kwa cheo na daraja au kiroho na halimaanishi kuinuliwa kimwili.

Soma aya zifuatazo:

(a) 7:177; (b) 19:58; (c) 24:37; 35:11; 3:56; 40:16; 49:3; 52:6; 56:35; (d) 80:15; (e) 56:4; (f) 58:12; (g) 4:159; 88:14.

Pia Mtume s.a.w. aliwahi kusema:

اِذَا تَوَاضَعَ الْعَبْدُ رَفَعَهُ اللّٰهُ اِلٰى السَّمَآءِ السَّابِعَةِ

Mtu anapokuwa mnyenyekevu, Allah Humnyanyua hadi mbingu ya saba. (Kanzul Ummal).

b. كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ الْمَوْتِ ثُمَّ اِلَيْنَا تُرْجَعُوْنَ

Kila nafsi itaonja mauti, kisha mtarudishwa Kwetu. (29:58).

7. وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِّنْ قَبْلِكَ الْخُلْدَ اَفَ ئِنْ مِّتَّ

فَهُمُ الْخٰلِدُوْنَ۝

Nasi hatukumfanya mwanadamu yeyote wa kabla yako aishi milele. Basi kama ukifa wao wataishi milele? (21:35).

6. وَلَكُمْ فِى الْاَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَّمَتَاعٌ اِلٰى حِيْنٍ ۝

... Na kao lenu litakuwa katika ardhi na posho kwa muda. (7:25).

7. قَالَ فِيْهَا تَحْيَوْنَ وَفِيْهَا تَمُوْتُوْنَ وَمِنْهَا تُخْرَجُوْنَ

Akasema: Mtaishi humo na mtafia humo, na mtatolewa humo. (7:26).

8.۝ بِالصَّلٰوةِ وَالزَّكٰوةِ مَا دُمْتُ حَيًّا وَاَوْصٰنِيْ

Ameniusia Sala na Zaka maadam ningali hai (19:32).

9. وَالسَّلٰمُ عَلَىَّ يَوْمَ وُلِدْتُّ وَ يَوْمَ اَمُوْتَ وَيَوْم اُبْعَثُ حَيًّا

Na amani iko juu yangu siku niliyozaliwa na siku nitakayokufa (19:34). na siku nitakayofufuliwa hai.

10.وَالَّذِيْنَ يَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ لَا يَخْلُقُوْنَ شَيْئاً

وَّهُمۡ يُخۡلَقُوۡنَ

اَمۡوَاتٌ غَيۡرُ اَحۡيَآءٍ وَمَايَشۡعُرُوۡنَ اَيَّانَ يُبۡعَثُوۡنَ

Na wale ambao wanawaita badala ya Mwenyezi Mungu hawaumbi chochote, bali wao wameumbwa; Ni wafu, si wazima, na hawajui watafufuliwa lini. (16:21-22).

11. وَجَعَلۡنَا ابۡنَ مَرۡيَمَ وَاُمَّهٗۤ اٰيَةً وَّاٰوَيۡنَا هُمَاۤ اِلٰى رَبۡوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ وَّمَعِيۡنٍ

Na Tulimfanya mwana wa Mariamu na mama yake kuwa Ishara, na Tukawapa makimbilio mahali palipoinuka penye starehe na chemchem. (23:51).

## HADITHI JUU YA KIFO

1. لَوۡ كَانَ مُوۡسٰى وَ عِيۡسٰى حَيَّيۡنِ لَمَا وَسِعَهُمَا اِلَّا اتِّبَاعِىۡ

Lau kama Musa na Isa wangelikuwa hai, wasingelikuwa na njia ila kunifuata. (*Zurqani*, jal. 6. uk. 54 na *Ibne Katheer* Jal. 2 uk. 246).

2. اَنَّ عِيۡسَى بۡنَ مَرۡيَمَ عَاشَ مِائَةً وَعِشۡرِيۡنَ سَنَةً

Hakika Isa mwana wa Mariamu aliishi miaka mia moja na ishirini (*Kanzul Ummal* jal. 6 uk. 160 na *Hujajul Karamah* uk. 428).

## 3. Masihi wa Musa na Masihi wa Muhammad s.a.w. ni watu wawili tofauti wenye sura mbalimbali:

a. عَنِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللّٰهُ عَنْهُمَا قَالَ قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَأَيْتُ عِيْسٰى وَمُوْسٰى وَ اِبْرَاهِيْمَ فَاَمَّا عِيْسٰى فَاَحْمَرُ جَعْدٌ عَرِيْضُ الصَّدْرِ

Abdullah bin Umar r.a. anasimulia kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. alisema: Niliwaona Isa, Musa na Ibrahimu, ama Isa alikuwa mwekundu mwenye nywele za kujisokota na mwenye kifua kipana. *(Bukhari kitaabul Anbiyaa, baab wadhkur fil kitaab Maryam).*

b. عَنْ عَبْدِ اللّٰهِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللّٰهُ عَنْهُمَا اَنَّ رَسُوْلَ اللّٰهِ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ اَرَانِيْ اللَّيْلَةَ عِنْدَ الْكَعْبَةِ فَرَاَيْتُ رَجُلًا اٰدَمَ كَاَحْسَنِ مَا اَنْتَ رَاءٍ رَجُلًا مِنْ اُدْمِ الرِّجَالِ لَهٗ لِمَّةٌ كَاَحْسَنِ مَا اَنْتَ رَاءٍ مِنَ

اللِّمَمِ قَدۡ رَجَّلَهَا فَهِيَ تَقۡطُرُ مَاءً مُتَّكِأً عَلٰى رَجُلَيۡنِ
... يَطُوۡفُ بِلۡبَيۡتِ فَسَاَلۡتُ مَنۡ هٰذَا فَقِيۡلَ الۡمَسِيۡحُ

Abdullah bin Umar r.a. anasimulia kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. alisema: Usiku mmoja niliona (katika ndoto) karibu na kaaba mtu mwenye rangi ya ngano, mtu mzuri sana miongoni mwa wenye rangi ya ngano, alikuwa na nywele ndefu, nywele nzuri kati ya nywele zilizonyooka, kana kwamba maji yanatiririka kutoka nywele zake na amewategemea watu wawili, anazunguka Alkaaba. Niliuliza huyu ni nani? Niliambiwa kwamba huyu ni Masihi. (*Bukhari, kitaabul libaas baab ju'ud).*

## WAFU HAWARUDI DUNIANI.

1. وَحَرٰمٌ عَلٰى قَرْيَةٍ اَهْلَكْنٰهَآ اَنَّهُمْ لَايَرْجِعُوْنَ

"Na ni haramu kwa mji Tulioungamiza ya kwamba wao hawatarejea" (21:96).

2. ثُمَّ اِنَّكُمْ بَعْدَ ذٰلِكَ لَمَيِّتُوْنَ
ثُمَّ اِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ تُبْعَثُوْنَ

"Kisha hakika ninyi baada ya hayo ni wenye kufa. Kisha hakika ninyi siku ya Kiyama mtafufuliwa." (23:16-17).

3. حَتّٰٓى اِذَا جَآءَ اَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ارْجِعُوْنِ
لَعَلِّىْٓ اَعْمَلُ صَالِحًا فِيْمَا تَرَكْتُ كَلَّا اِنَّهَا كَلِمَةٌ
وَمِنْ وَّرَآئِهِمْ بَرْزَخٌ اِلٰى يَوْمِ يُبْعَثُوْنَ هُوَ قَآئِلُهَا

"Hata yanapomfikia mmoja wao mauti, husema: Mola wangu unirudishe: Ili nifanye mema katika yale niliyoyaacha. Hapana! Hakika hili ni neno tu analolisema; na nyuma yao iko kinga mpaka siku watakapofufuliwa." (23:100-101).

4. اَللّٰهُ يَتَوَفَّى الْاَنْفُسَ حِيْنَ مَوْتِهَا وَالَّتِى لَمْ

تَمُتْ فِىْ مَنَامِهَا فَيُمْسِكُ الَّتِىْ قَضٰى عَلَيْهَا الْمَوْتَ

Mwenyezi Mungu hutakabadhi roho wakati wa mauti yao, na zile zisizokufa, katika usingizi wao. Basi huzizuia zile Alizozikidhia mauti ..." (39:43).

5. Abdullah r.a. sahaba mmoja wa Mtukufu Mtume s.a.w. aliuawa katika vita vya dini. Mtume Mtukufu s.a.w. alisema kumwambia Jabir - mtoto wa sahaba huyo aliyeuawa kwamba: Mwenyezi Mungu amezungumza na baba yako na kumwambia: "Niombe chochote ukipendacho nitakupatia." Abdullah aliomba; Ee Allah, unihuishe ili nikauawe tena katika njia yako. Mwenyezi Mungu alimwambia kwamba: "Jambo hili nimepitisha tayari kwamba wafu hawarudi tena duniani" (*Jamee Tirmidhi - Mishakaat Mujtabai Bab Jamiul Manaqib* uk. 579).
6. Mtu mmoja alifariki, watu wake walimjia Mtume Mtukufu s.a.w. kuomba kwamba amuombee ili afufuke. Mtume Muhammad s.a.w. aliwaambia kwamba ombeni maghofira kwa mtu wenu na mzikeni (*Sahihi Muslim Mishkaat Mujtabai Baab Maa yahillu likullihi* uk. 360).

7. Hata Biblia inakataa jambo hili.
Mfu hatafufuka wala hatarudi tena nyumbani kwake, wala mahali pake hapatamjua tena. (Ayubu 7:9-10).

## UTUME UNAENDELEA KATIKA ISLAM

يٰبَنِىۡۤ اٰدَمَ اِمَّا يَاۡتِيَنَّكُمۡ رُسُلٌ مِّنۡكُمۡ
يَقُصُّوۡنَ عَلَيۡكُمۡ اٰيٰتِىۡ فَمَنِ اتَّقٰى
وَاَصۡلَحَ فَلَا خَوۡفٌ عَلَيۡهِمۡ وَلَا هُمۡ يَحۡزَنُوۡنَ

Enyi wanadamu, bila shaka watawafikieni Mitume kutoka miongoni mwenu, watawaelezeni Aya Zangu. Basi atakayeogopa na kufanya wema, haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika. (7:36).

*Yaatiyanna na Yaqussuuna ni fe'l Mudhaari'u* ikimaanisha wakati ulipo na wakati ujao.

Enyi wanadamu - 7:27; 7:28; 7:32. يٰبَنِىۡۤ اٰدَمَ

Qul - 7:30; 7:33; 7:34. قُلۡ

Immaa 2:39; 20:124; 40:78; 13:41. اِمَّا

وَقَالَ الرَّسُوۡلُ يٰرَبِّ اِنَّ قَوۡمِى
اتَّخَذُوۡا هٰذَا الۡقُرۡاٰنَ مَهۡجُوۡرًا

(a). Na Mtume atasema: Ee Mola wangu, hakika watu wangu wameifanya Kurani hii kuwa kitu kilichowachwa. (25:31).

2. اَللّٰهُ يَصۡطَفِىۡ مِنَ الۡمَلٰٓئِكَةِ رُسُلًا وَّمِنَ النَّاسِ اِنَّ اللّٰهَ سَمِيۡعٌ بَصِيۡرٌ

Mwenyezi Mungu Huchagua Mitume miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu: kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Asikiaye, Aonaye. (22:76).

3. مَاكَانَ اللّٰهُ لِيَذَرَ الۡمُؤۡمِنِيۡنَ عَلٰى مَآ اَنۡتُمۡ عَلَيۡهِ حَتّٰى يَمِيۡزَ الۡخَبِيۡثَ مِنَ الطَّيِّبِ وَمَاكَانَ اللّٰهُ لِيُطۡلِعَكُمۡ عَلٰى الۡغَيۡبِ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ يَجۡتَبِىۡ مِنۡ رُّسُلِهٖ مَنۡ يَّشَآءُ

Haimpasi Mwenyezi Mungu kuwaacha waaminio katika hali mliyo nayo mpaka Apambanue mbaya katika mwema; wala haimpasi Mwenyezi Mungu kuwajulisheni mambo ya ghaibu, bali Mwenyezi Mungu huchagua katika Mitume Wake Amtakaye. (3:180).

4. وَمَنۡ يُّطِعِ اللّٰهَ وَالرَّسُوۡلَ فَاُولٰٓئِكَ مَعَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمَ اللّٰهُ عَلَيۡهِمۡ مِّنَ النَّبِيّٖنَ وَالصِّدِّيۡقِيۡنَ وَالشُّهَدَآءِ وَالصّٰلِحِيۡنَ وَحَسُنَ اُولٰٓئِكَ

رَفِيقًا ☆ ذٰلِكَ الْفَضْلُ مِنَ اللّٰهِ وَكَفٰى بِاللّٰهِ عَلِيْمًا

Na Mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao ni miongoni mwa wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu - Manabii na Masidiki na Mashahidi na Masalih; na hao ndio Hiyo ni fadhili itokayo kwa Mwenyezi Mungu; marafiki wema. na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mjuzi. (4:70 - 71).

a. وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖٓ اُولٰٓئِكَ
هُمُ الصِّدِّيْقُوْنَ وَالشُّهَدَآءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ

Na wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake hao ndio masiddiki na mashahidi mbele ya Mola wao. (57:20). Neno *maa* (pamoja) pia linaweza kutumika kwa maana ya *min* (miongoni).

(a). وَتَوَفَّنَا مَعَ الْاَبْرَارِ

......... Na utufishe pamoja na na watu wema. (3:194).

Juu ya Iblis inasemwa:

(b). اَبٰٓى اَنْ يَكُوْنَ مَعَ السّٰجِدِيْنَ

Akakataa kuwa pamoja na waliotii (Hijri: 15:32).

(c). لَمۡ يَكُنۡ مِّنَ السّٰجِدِيۡنَ

Hakuwa miongoni mwa waliotii (Al-Aaraf; 7:12).

5. وَاِذۡ اَخَذَ اللّٰهُ مِيۡثَاقَ النَّبِيّٖنَ لَمَاۤ اٰتَيۡتُكُمۡ مِّنۡ كِتٰبٍ وَّحِكۡمَةٍ ثُمَّ جَآءَكُمۡ رَسُوۡلٌ مُّصَدِّقٌ لِّمَا مَعَكُمۡ لَتُؤۡمِنُنَّ بِهٖ وَلَتَنۡصُرُنَّهٗ قَالَ ءَاَقۡرَرۡتُمۡ وَاَخَذۡتُمۡ عَلٰى ذٰلِكُمۡ اِصۡرِىۡ قَالُوۡۤا اَقۡرَرۡنَا قَالَ فَاشۡهَدُوۡا وَاَنَا مَعَكُمۡ مِّنَ الشّٰهِدِيۡنَ

Na (kumbukeni) Aliposhika Mwenyezi Mungu ahadi kwa Manabii: Nikiisha wapeni Kitabu na hekima, kisha awafikieni Mtume msadikishaji wa yale yaliyo pamoja nanyi, ni juu yenu kumwamini na kumsaidia. Akasema, Je, mmekubali na kushika agizo Langu juu ya hayo? Wakanena: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika mashahidi. (3:82).

a. وَاِذۡ اَخَذۡنَا مِنَ النَّبِيّٖنَ مِيۡثَاقَهُمۡ وَمِنۡكَ وَمِنۡ نُّوۡحٍ وَّاِبۡرٰهِيۡمَ وَمُوۡسٰى وَعِيۡسَى ابۡنِ مَرۡيَمَ وَاَخَذۡنَا مِنۡهُمۡ مِّيۡثَاقًا غَلِيۡظًا

Na Tulipoahidiana na Manabii na wewe, na Nuhu na Ibrahimu na Musa na Isa mwana wa Mariamu na Tuliahidiana nao ahadi ngumu. (33:8).

6. وَلَقَدْ جَآءَكُمْ يُوْسُفُ مِنْ قَبْلُ بِالْبَيِّنٰتِ فَمَا زِلْتُمْ فِىْ شَكٍّ مِّمَّا جَآءَكُمْ بِهٖ حَتّٰىٓ اِذَا هَلَكَ قُلْتُمْ لَنْ يَبْعَثَ اللّٰهُ مِنْ بَعْدِهٖ رَسُوْلًا كَذٰلِكَ يُضِلُّ اللّٰهُ مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ مُّرْتَابُ

Na bila shaka zamani aliwafikieni Yusuf kwa dalili zilizo wazi, lakini ninyi mliendelea katika shaka kwa yale aliyowaleteeni; mpaka alipofariki mkasema: Mwenyezi Mungu Hataleta kabisa Mtume baada yake. Kama hivyo Mwenyezi Mungu Huthubutisha upotevu wa yule aliyepita kiasi, mwenye shaka. (40:35).

a. مَا يُقَالُ لَكَ اِلَّا مَا قَدْ قِيْلَ لِلرُّسُلِ مِنْ قَبْلِكَ

Hutaambiwa maneno ila yale yale tu waliyoambiwa Mitume wa kabla yako (41:44).

b. وَاَنَّهُمْ ظَنُّوْ كَمَا ظَنَنْتُمْ اَنْ لَّنْ يَبْعَثَ اللّٰهُ اَحَدًا

Na kwa hakika wao walidhani kama mlivyodhani ninyi ya kuwa Mwenyezi Mungu Hatamtuma (Mtume) yeyote. (72:8).

## KUENDELEA KWA UTUME KATIKA HADITHI

a. عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِىَ اللّٰهُ عَنْهُ قَالَ لَمَّا مَاتَ
اِبْرَاهِيْمُ ابْنُ رَسُوْلِ اللّٰهِ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّم
صَلّٰى رَسُوْلِ اللّٰهِ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ
وَقَالَ اِنَّ لَهٗ مُرْضِعًا فِى الْجَنَّةِ وَلَوْ عَاشَ لَكَانَ صِدِّيْقًا نَبِيًّا

(Ibraimu bin Muhammad s.a.w.) kama angeishi angekuwa Mtume Mkweli). (Ibn Majah Kitaabul Janaaiz).

b. اَبُوْ بَكَرٍ خَيْرُ النَّاسِ بَعْدِىْ اِلَّا اَنْ يَّكُوْنَ نَبِىٌّ

Abubakar ni mbora wa Umma huu isipokuwa kama atokezee nabii. (Dhailamy).

c. فَاِنِّىْ اٰخِرُ الْاَنْبِيَاءِ وَاِنَّ مَسْجِدِىْ اٰخِرُ الْمَسَاجِدِ

Bila shaka mimi ni mwisho wa Manabii na msikiti wangu ni mwisho wa misikiti. (Muslim Kitaabul Hajj).

d. اَبُوْ بَكَرٍ اَفُضَلُ هٰذِهِ الْاُمَّةِ اِلَّا اَنْ يَّكُوْنَ نَبِيٌّ

Abubakar ..........

f. لَا مَهْدِيَّ اِلَّا عِيْسَى بْنُ مَرْيَمَ

Hakuna Mahdi ila Issa. (Ibni Majah Kitaabul Fitan, Baab Shiddatuzzaman).

g. يُوْشَكُ مَنْ عَاشَ مِنْكُمْ اَنْ يَلْقٰى عِيْسَى بْنُ مَرْيَمَ اِمَامًا مَهْدِيًّا حَكَمًا عَدْلًا يَكْسِرُ الصَّلِيْبَ وَيَقْتُلُ الْخِنْزِيْرَ

Yeyote atakayekuwa hai miongoni mwenu atamkuta Isa mwana wa Mariamu akiwa ni Imam Mahdi na hakimu muwadilifu. (Masnad Ahmad bin Hambal Jal. 2. uk. 411).

h. لَيْسَ بَيْنِىْ وَبَيْنَهٗ نَبِيٌّ وَاِنَّهٗ نَازِلٌ

Hakuna Nabii baina yangu Mimi na yeye (Masihi) na hakika atakuja. (Abu Daud Kitaabul Malaahim).

i. يَبْعَثُ عِيْسٰى ابْنِ مَرْيَمَ

Atainuliwa Isa bin Maryam ........

j. قُوْلُوا انَّهٗ خَاتَمُ الْاَنْبِيَاءِ
وَلَا تَقُوْلُوْا لَا نَبِیَّ بَعْدَهٗ

Bibi Aisha alisema kwamba semeni kuwa yeye ni Khatamul Ambiyaa wala msiseme kamwe kwamba hakuna Nabii baada yake. (Takmila Majmail-Bihaar uk. 85; Al Durral Mansoor cha Suyyuti Jl. 5 uk. 204).

k. النُّبُوَّةُ سَارِيَةٌ اِلٰی يَوْمِ الْقِيَامَةِ فِیْ
الْخَلْقِ وَاِنْ كَانَ التَّشْرِيْعَ قَدْانْقَطَعَ

Sheikh Muhiyuddin Ibni Arabi amesema kwamba utume utaendelea mpaka siku ya kiyama katika viumbe na ingawaje utume wa sheria umekatika. (Futuuhatul Makiyya Jal. uk. 100).

## UKHALIFA KATIKA ISLAM

1. وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيۡنَ اٰمَنُو مِنۡكُمۡ وَعَمِلُو ا
الصّٰلِحٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِى الۡاَرۡضِ كَمَا
اسۡتَخۡلَفَ الَّذِيۡنَ مِنۡ قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُم
دِيۡنَهُمُ الَّذِىۡ ارۡتَضٰى لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمۡ مِّنۡ بَعۡدِ
خَوۡفِهِمۡ اَمۡنًا يَعۡبُدُوۡنَنِىۡ لَا يُشۡرِكُوۡنَ بِىۡ شَيۡـًٔا
وَ مَنۡ كَفَرَ بَعۡدَ ذٰلِكَ فَأُولٰٓئِكَ هُمُ الۡفٰسِقُوۡنَ

Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na cho chote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri. (24:56).

a. وَاِذۡ قَالَ رَبُّكَ لِلۡمَلٰٓئِكَةِ اِنِّىۡ جَاعِلٌ فِىۡ الۡاَرۡضِ
خَلِيۡفَةٌ

Hakika mimi nitamweka Khalifa katika ardhi (2:31).

b. يٰدَاوٗدَ اِنَّا جَعَلْنٰكَ خَلِيْفَةً فِى الْاَرْضِ

Ewe Daudi hakika Tumekujaalia kuwa Khalifa ardhini, (38:27).

2. ثُمَّ تَكُوْنُ خِلَافَةٌ عَلٰى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ

Zama za mwisho ukhalifa utapatikana chini ya msingi wa Unabii. (Musnad Ahmad Jal. 4 uk. 273).(Mishkaat baab Indhaar wa Tahdhir).

3.

Baada yangu mimi ukhalifa utadumu kwa miaka 30 tu. (Mishkaatul Masabih, Kitabul fitn)

4. قَالَ تَلْزَمُ جَمَاعَةُ الْمُسْلِمِيْنَ وَاِمَامَهُمْ
قُلْتُ فَاِنْ لَمْ يَكُنْ لَهُمْ جَمَاعَةٌ وَلَا اِمَامَ
قَالَ فَاعْتَزِلْ تِلْكَ الْفِرٰقُ كُلَّهَا

Ni amri ya Mtume s.a.w. kujiunga na Jumuiya ya Waislamu yenye Imamu mmoja na kama hakuna Jumuiya ya Imam basi tumekatazwa kujiunga na mahali popote. (Bukhari Kitaabul

Manaqiib, Mishkaat Baabul Fitan).

اَفَمَنۡ كَانَ مُؤۡمِنًا كَمَنۡ كَانَ فَاسِقًا لَايَسۡتَوٗنَ

Je! mumini anaweza kuwa sawa na yule aliye fasiki? Hawawi sawa. (32:19).

## MASIHI NA MAHDI KATIKA ISLAM

1. صِرَاطَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ غَيۡرِ الۡمَغۡضُوۡبِ عَلَيۡهِمۡ وَلَاالضَّآلِّيۡنَ

... Siyo ya wale walioghadhibikiwa wala ya wale waliopotea. (1:7).

Waliokasirikiwa ni Mayahudi, kwa sababu ya kumkataa Masihi wa umma wa Musa a.s. Sisi Waislamu tumefundishwa kujiepusha na njia yao. Yaani Masihi katika Umma wa Mtume Muhammad s.a.w. atakuja, tusiwe miongoni mwa waliomkufuru.

2. اِنَّا اَرۡسَلۡنَآ اِلَيۡكُمۡ رَسُوۡلًا شَهِدًا عَلَيۡكُمۡ

كَمَآ اَرۡسَلۡنَآ اِلٰی فِرۡعَوۡنَ رَسُوۡلاً

Hakika sisi tumewateremshieni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama Tulivyompeleka Mtume kwa Farauni.(73:16).

Katika Aya hii Mtume Muhammad s.a.w. amefananishwa na Nabii Musa a.s.. Kama baada ya Nabii Musa a.s. katika karne ya 14 Masihi wake alikuja, vile vile ilikuwa lazima baada ya Mtume Muhammad s.a.w. katika karne 14 Masihi wa Kiislamu aje.

3. هُوَ الَّذِیۡۤ اَرۡسَلَ رَسُوۡلَهٗ بِالۡهُدٰی وَدِیۡنِ الۡحَقِّ لِیُظۡهِرَهٗ عَلَی الدِّیۡنِ کُلِّهٖ وَلَوۡ کَرِهَ الۡمُشۡرِکُوۡنَ

Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa mwongozo na kwa dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote ijapokuwa washirikina wachukie. (61:10).

(a) Ushindi huu utatokea wakati wa ujaji wa Mahdi (Kitabu cha wasunni (Tafsir Ibn Jarir maelezo juu ya aya ya juu).

(b) Aya hii iliteremka kuhusu Al Qaim yaani Imam Mahdi (Bihar ul Anwar, maelezo ya aya ya juu).

(c). Katika aya hii Mtume aliyetajwa ni Imam Mahdi (Ghayat ul Maqsood Jl. 2 uk. 123).

(d) Tafsiri Qummi (maelezo ya aya ya 9:33).

(e) Tafsir Saafi (Maelezo ya aya ya 9:33).

4. وَلَمَّا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مَثَلًا اِذَا قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّوْنَ

Na anapotajwa mwana wa Mariamu kwa namna ya mfano ndipo watu wako wanaupigia kelele. (43:58).

a. يُوْشَكُ مَنْ عَاشَ مِنْكُمْ اَنْ يَلْقٰى عِيْسَى بْنُ مَرْيَمَ اِمَامًا مَهْدِيًّا حَكَمًا عَدْلًا يَكْسِرُ الصَّلِيْبَ وَيَقْتُلُ الْخِنْزِيْرَ

Yeyote ambaye atabaki miongoni mwenu atakutana na Isa mwana wa Mariamu akiwa Imam Mahdi na hakimu mwadilifu. (*Musnad Ahmad bin Hambal* Jl. 2 uk. 411).

5. لَا مَهْدِيَّ اِلَّا عِيْسَى بْنُ مَرْيَمَ

Hakuna Mahdi ila Isa - Masihi aliyeahidiwa.
*(Ibne Majah Baab Shiddatuzzaman).*

6. Imam Mahdi atafanana na Isa bin Mariamu zaidi kuliko watu wote *(Bihar ul Anwar usimulizi wa Abu Dardaa).*

7. Shah Waliullah Mujadid wa karne ya 12 alisema kwamba Mwenyezi Mungu ameniambia kuwa Kiyama ni karibu na Mahdi yupo tayari kutumwa.
*(Tafhimat e Ilahiyya Jl. 2 uk. 123).*

8. Imam Muhammad Bakir a.r. alisema kwamba: Ambaye anatupenda ndiye miongoni mwa Ahlul Bait.
(Tafsir Majmaul Bayan na Tabri aya 14:37).

9. Mtume Mtukufu s.a.w. alisema kwamba:
Salman Mwajemi ni miongoni mwa Ahlul Bait. (Tafsir Majmaul Bayan na Tabri aya 11:47).

10. Imam Mahdi atadai kuwa Adam, Nuhu, Musa, Isa na Muhammad s.a.w. na Maimamu wa Ahlul Bait. (Biharul Anwar jl. 13 uk. Na. 33).

11. Imam Mahdi atazaliwa siku ya Ijumaa (Biharul Anwar jl. 13 uk. 173.

12. Imam Mahdi atafundishwa katika usiku mmoja. (*Biharul Anwar* jl. 37 uk. 21).
Seyyidna Ahmad a.s. katika usiku mmoja alifundishwa misingi arubaini elfu ya maneno ya Kiarabu na kuanzia hapo aliandika vitabu 25 katika lugha ya Kiarabu.

عَنْ مُحَمَّدِ بْنِ عَلِيِّ قَالَ اِنَّ لِمَهْدِيِّنَا اٰيَتَيْنِ

لَمْ تَكُوْنَا مُنْذُ خَلْقِ السَّمٰوَاتِ وَالْاَرْضِ
تَنْكَسِفُ الْقَمَرُ لِاَوَّلِ لَيْلَةٍ مِنْ رَمَضَانَ
وَتَنْكَسِفُ الشَّمْسُ فِی النِّصْفِ مِنْهُ
وَلَمْ تَكُوْنَامُنْذُ خَلْقِ السَّمٰوَاتِ وَالْاَرْضِ

13. Wakati wa Imam Mahdi kwa ajili ya ukweli wake jua na mwezi vitapatwa katika tarehe maalum ndani ya mwezi wa Ramadhani (*Furu-e- Kafi Kitabu Rodha* uk. 100).

Mwezi ulipatwa tarehe 13 ya Ramadhani (21 March 1894 siku ya Jumatano na jua likapatwa tarehe 28 ya mwezi wa Ramadhani 6 April 1894 siku ya Ijumaa). (Civil and Military Gazete Lahore - 7 April 1994).

14. Mtume Muhammad s.a.w alisema kwamba: (a) Mtu ambaye atamkataa Mahdi atakuwa amenikataa mimi na ambaye atamuunga mkono atakuwa ameniunga mkono mimi. (Biharul Anwar jl. 13 uk. 13).

فَاِذَا رَأَيْتُمُوْهُ فَبَايِعُوْهُ وَلَوْ حَبْوًا عَلَى
الثَّلْجِ فَاِنَّهٗ خَلِيْفَةُ اللّٰهِ الْمَهْدِىُّ

(b) Wakati Imam Mahdi aje mjiunge naye ingawa njia iwe

ngumu (hata kwa kutambaa juu ya theluji) kwa maana yeye ni Mahdi - Khalifa wa Mwenyezi Mungu.
(c) Basi msalimieni kwa kusema kwamba Ee hazina ya Elimu na jukwaa la utume, Salamu na amani kwako. (Biharul Anwar jl. 13).

Seyyidna Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wa Qadiani mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ndiye mdai wa pekee ambaye alama zote zimetimia kwake. Ni yeye ambaye amedai kwamba ametumwa na Mwenyezi Mungu. Yeye ni Masihi lakini hajashuka kutoka msalabani. Yeye ni Mahdi lakini bila upanga wa vita.

# UKWELI WA SEYIDNA AHMAD A.S.

1.فَقَدۡ لَبِثۡتُ فِيۡكُمۡ عُمُرًا مِّنۡ قَبۡلِهِ اَفَلَا تَعۡقِلُوۡنَ

Hakika nimekwisha kaa kati yenu umri mwingi, je, hamfahamu (10:17).

NB. Dalili ni ukweli kabla ya kudai.

Seyyidna Ahmad a.s. alitoa tambio kwamba maisha yake kabla ya kudai ni safi sana kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu, hakuna yeyote ambaye anaweza kuleta lawama yoyote. Na hii ni dalili ya kutosha kwa wenye akili.

(Tadhkiratush-shahadatain).

Sheikh Muhammad Hussein wa Batala alisema mapema kwamba: Seyyidna Ahmad a.s. sawa na marafiki na wapinzani ni mtu wa kufuata sheria sana sana na mchamungu na mkweli.

(Isha-atusunnah Jal. 7 uk. 9).

2. وَلَوۡ تَقَوَّلَ عَلَيۡنَا بَعۡضَ الۡاَقَاوِيۡلِ

لَاَخَذۡنَا مِنۡهُ بِالۡيَمِيۡنِ

ثُمَّ لَقَطَعۡنَا مِنۡهُ الۡوَتِيۡنَ

فَمَا مِنۡكُمۡ مِّنۡ اَحَدٍ عَنۡهُ حٰجِزِيۡنَ

Na kama (Mtume) angelizua juu yetu baadhi ya maneno, Bila shaka Tungalimshika kwa mkono wa kuume,  Kisha kwa hakika Tungalimkata mshipa mkubwa (wa moyo).
Na hakuna ye yote katika ninyi ambaye angeweza kumkinga Tusimfikie. (69:45-48).

NB. Mtume muongo anauwawa na anaangamizwa.
Imam Ibni Kayyim amesema kwamba mtume muongo hapewi baada ya madai yake muda wa kuishi sawa na miaka 23 (sawa na miaka ya Mtume Muhammad s.a.w. (Zaadul Maad jal. 1 uk. 500).

3. وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا اَوْ كَذَّبَ بِاٰيٰتِهٖ اِنَّهٗ لَايُفْلِحُ الظّٰلِمُوْنَ

3. Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye uwongo Mwenyezi Mungu au azikadhibishaye Ishara Zake? Hakika wadhalimu hawatafaulu. (6:22).

Biblia pia inakubali kwamba Mtume mwongo atauwawa (Kumb.13:5).
Mtume muwongo hawezi kuishi miaka 23 baada ya madai yake kama alivyoishi Mtume wetu Muhamamd s.a.w.
Vitabu vifuatavyo vimetaja juu ya jambo hili:

1. Sharha Aqaid e nasfi uk. 100 cha Masunni.
2. Sharha Nabras uk. 444.
3. Nabras chapa ya Mirth uk. 444.
4. Zadul Maad cha Imam Ibne Kayyum Jal. 1uk 500.
5. Tafsiri Ibne Jarir ya Allama Fakhruddin Razi Jl. 8 uk. 291
6. Tafsir Ibne Jarir ya Imam Jaffar Tabri Jl. 29 uk. 42 na 37.
7. Tafsir Sanai ya Sh. Sanaullah uk. 17.
8. Tafsiri Rooh ul Bayyan jl. 4 uk. 482.
9. Tafsir Kashshaf uk. 1824.
10. Tafsiri Ibne Kathir Jl. 10 uk. 71.
11. Tafsir Fathul Bayan Jl. 10 uk. 37.
12. Tafsir Jalalain Mujtabai uk. 470.
13. Shahah Alalbidawi Jal. 8 uk. 241

14. Al Saraj ul Munir ya Sh. Khatib Baghdadi Jl. 4 uk. 363.

4. كَتَبَ اللّٰهُ لَاَغْلِبَنَّ اَنَا وَرُسُلِی

Mwenyezi Mungu Amekwisha andika: Bila shaka Nitashinda Mimi na Mitume Wangu! (58:22).

5. اِنَّا لَنَنْصُرَ رُسُلَنَا وَالَّذِیْنَ اٰمَنُوْا فِی

الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُوْمُ الْاَشْهَادُ

Bila shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi (40:52).

4. عٰلِمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عِلٰى غَيْبِهٖ اَحَدًا اِلَّا مَنِ ارْتَضٰى مِنْ رَّسُوْلٍ

Yu Mjuzi wa yasiyoonekana, na Hampi ye yote uwezo wa kiutawala juu ya milki Yake ya mambo yasiyoonekana. Isipokuwa yule Anayemchagua kuwa Mtume Wake. Na mbele yake na nyuma yake hutembea malaika kama walinzi. (72:27-28).

NB. Tabiri za Seyyidna Ahmad a.s.

(a) Lekhram (b) Dr. Dowie (c) Mwana Aliyeahidiwa

(d) Ujumbe utafika pembe zote za duniani n.k

5. هُوَ الَّذِىْ بَعَثَ فِى الْاُمِّيّٖنَ رَسُوْلًا مِّنْهُمْ يَتْلُوْا عَلَيْهِمْ اٰيٰتِهٖ وَيُزَكِّيْهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ وَاِنْ كَانُوْا مِنْ قَبْلُ لَفِىْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ وَاٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوْا بِهِمْ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ

Yeye ndiye Aliyemwinua Mtume katika watu wasiojua kusoma, atokaye miongoni mwao, anawasomea Aya Zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima, na ingawa kabla kwa hakika walikuwa katika upotevu dhahiri -
Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao; na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima. (62:3-4).

NB. Mtume Muhammad s.a.w. atatumwa kati ya watu wengine wasiokuwa Waarabu.

عَنْ اَبِىْ هُرَيْرَةَ رَضِىَ اللّٰهُ عَنْهُ قَالَ كُنَّا جُلُوْسًا
عِنْدَ النَّبِىِّ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّم
سُوْرَةُ الْجُمُعَةِ فَلَمَّا قَرَأَ اِذْ نَزَلَتْ عَلَيْهِ
وَاٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوْا بِهِمْ قَالَ رَجُلٌ
مَنْ هٰؤُلَآءِ يَارَسُوْلَ اللّٰهِ فَلَمْ يُرَاجِعْهُ النَّبِىُّ
صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ حَتّٰى سَأَلَهٗ مَرَّةً اَوْ مَرَّتَيْنِ
اَوْ ثَلَاثًا قَالَ وَفِيْنَا سَلْمَانُ الْفَارِسِىُّ قَالَ فَوَضَعَ
النَّبِىُّ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَدَهٗ عَلٰى سَلْمَانَ
ثُمَّ قَا لَ لَوْ كَانَ الْاِيْمَانُ عِنْدَ الثُّرَيَّا لَنَا
لَهٗ رَجُلٌ اَوْ رِجَالٌ مِنْ هٰؤُلَآءِ

Mtume s.a.w. akifafanua aya iliyopita alisema: Wakati imani itapotea mtu au watu kutoka kabila la Salman Muajemi ataileta. (*Bukhari Kitaab Tafsiir; Muslim Kitaabul Fadhaail*).

عَنْ مُصْعَبَ ابْنِ عَبْدِ اللّٰهِ قَالَ قَالَ رَسُوْلُ اللّٰهِ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَلْمَانُ مِنَّا اَهْلِ الْبَيْتِ

Salman (Muajemi) ni miongoni mwa Ahlul Bait. (Mustadrak).

6. يٰحَسْرَةً عَلَى الْعِبَادِ مَايَأْتِيْهِمْ مِّنْ رَسُوْلٍ اِلَّا كَانُوْا بِهِ يَسْتَهْزِئُوْنَ

Ni sikitiko kwa watumishi: hakuwafikia Mtume yeyote ila walikuwa wanamfanyia mzaha. (36:31).

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِيْنَ حَتّٰى نَبْعَثَ رَسُوْلًا

Nasi si waadhibishao mpaka tumepeleka Mtume (17:16).

وَاِنْ مِّنْ قَرْيَةٍ اِلَّا نَحْنُ مُهْلِكُوْهَا قَبْلَ يَوْمِ الْقِيٰمَةِ اَوْ مُعَذِّبُهَا عَذَابًا شَدِيْدًا

Na hakutakuwa mji ila Sisi Tutauhilikisha kabla ya siku ya Kiyama au kuuadhibu adhabu kali. (17:59).

7.وَاِذۡ قَالَ عِيۡسَى ابۡنُ مَرۡيَمَ يٰبَنِىۡۤ اِسۡرَآءِيۡلَ
اِنِّىۡ رَسُوۡلُ اللّٰهِ اِلَيۡكُمۡ مُّصَدِّقًا لِّمَا بَيۡنَ
يَدَىَّ مِنَ التَّوۡرٰٮةِ وَمُبَشِّرًۢا بِرَسُوۡلٍ يَّاۡتِىۡ مِنۡۢ بَعۡدِى اسۡمُهٗۤ
اَحۡمَدُ

Na aliposema Isa bin Mariamu: Enyi wana wa Israeli, mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyo mbele yangu katika Taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakayefika nyuma yangu jina lake ni Ahmad; (61:7).

Katika Aya zilizopita Mitume wafuatao wametajwa:
Nabii Musa, Nabi Isa, Nabii aliyetajwa katika Taurati yaani Muhammad s.a.w. na Nabii Ahmad.

قَالُوۡا يٰقَوۡمَنَاۤ اِنَّا سَمِعۡنَا كِتٰبًا اُنۡزِلَ مِنۡۢ بَعۡدِ مُوۡسٰى

Wakasema: Enyi watu wetu, hakika Tumesikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa... (46:31).

اَفَمَنۡ كَانَ عَلٰى بَيِّنَةٍ مِّنۡ رَّبِّهٖ وَيَتۡلُوۡهُ
شَاهِدٌ مِّنۡهُ وَمِنۡ قَبۡلِهٖ كِتٰبُ مُوۡسٰٓى اِمَامًا وَّرَحۡمَةً

Basi je, anaweza kuwa mwongo, mtu ambaye ana uthibitisho ulio wazi kutoka kwa Mola wake, na ambaye ili kuthibitisha ukweli wake, shahidi mmoja kutoka Kwake atamfuata, na ambaye alitanguliwa na Kitabu cha Musa .... (11:18).

NB. Baada ya nabii Musa ilishushwa Zaburi na Injili na kabla ya Mtume Muhammad s.a.w. kilikuwako kitabu cha nabii Isa a.s. na nabii Daudi a.s.

عَنْ مُحَمَّدِ بْنِ عَلِيّ قَالَ اِنَّ لِمَهْدِيِّنَا اٰيَتَيْنِ
لَمْ تَكُوْنَا مُنْذُ خَلْقِ السَّمٰوَاتِ وَالْاَرْضِ
تَنْكَسِفُ الْقَمَرُ لِاَوَّلِ لَيْلَةٍ مِنْ رَمَضَانَ
وَتَنْكَسِفُ الشَّمْسُ فِى النِّصْفِ مِنْهُ
وَلَمْ تَكُوْنَامُنْذُ خَلْقِ السَّمٰوَاتِ وَالْاَرْضِ

Kwa ajili ya Mahdi wetu, jua na mwezi vitapatwa katika mwezi wa Ramadhani. Jua tarehe 28 na mwezi tarehe 13, na haijawahipo kutokea kuwa ni dalili kwa mdai yeyote wa unabii tokea kuumbwa kwa ulimwengu.

(Sunan Dar Qutnii Kitaabul Iidain Baab Swalaatul Khusuuf wal Kusuuf).

# MTUME MUHAMMAD S.A.W. KATIKA QUR'AN

وَمَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوْلٌ

Na siye Muhammad ila yu Mtume (3:145).

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ اَبَآ اَحَدٍ مِّنْ رِّجَالِكُمْ

Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu (33:41).

وَاٰمَنُوْ بِمَا نُزِّلَ عَلٰى مُحَمَّدٍ

... na wakaamini yaliyoteremshwa juu ya Muhammad (47:3

مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (48:30).

**Muhammad mfano wa Musa**

اِنَّـآ اَرْسَلْنَـآ اِلَيْكُمْ رَسُوْلًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَآ

اَرۡسَلۡنَآ اَلٰى فِرۡعَوۡنَ رَسُوۡلًا

Hakika Sisi Tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama Tulivyompeleka Mtume kwa Firauni (73:16).

**Mtume Muhammad ametajwa katika Torati**

اَلَّذِيۡنَ يَتَّبِعُوۡنَ الرَّسُوۡلَ النَّبِىَّ الۡاُمِّىَّ الَّذِى
يَجِدُوۡنَه مَكۡتُوۡبًا عِنۡدَهُمۡ فِى التَّوۡرٰةِ وَالۡاِنۡجِيۡلِ

Ambao wanamfuata Mtume, Nabii aliye Ummi, ambaye ambaye wao humkuta ameandikwa kwao katika Taurati na Injili (3:158).

## MENGINEYO

اَللّٰهُ اَعۡلَمُ حَيۡثُ يَجۡعَلُ رِسَالَتَه

Mwenyezi Mungu ndiye Ajuaye zaidi Atakapoweka utume wake. (6:125).

وَمَا اَنۡتَ بِمُسۡمِعٍ مَّنۡ فِى الۡقُبُوۡرِ

... nawe (Muhammad) huwezi kuwasikilizisha waliomo makaburini. (35:23).

فَاِنَّكَ لَا تُسۡمِعُ الۡمَوۡتَ

Bila Shaka huwezi kuwasikilizisha wafu (30:53).

## Utume bila Sheria

اِنَّـآ اَنۡزَلۡنَا التَّوۡرٰةَ فِيۡهَا هُدًى وَّنُوۡرٌ يَحۡكُمُ
بِهَا النَّبِيُّوۡنَ الَّذِيۡنَ اَسۡلَمُوۡا لِلَّذِيۡنَ هَادُوۡا
وَالرَّبّٰنِيُّوۡنَ وَالۡاَحۡبَارُ بِمَا اسۡتُحۡفِظُوۡا مِنۡ كِتٰبِ اللّٰهِ

Hakika Tuliteremsha Taurati yenye mwongozo na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia, kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu, (5:45).

اَفَعَصَيۡتَ اَمۡرِىۡ

Nabii Musa alimwambia ndugu yake Nabii Haruni. Je, umeasi amri yangu? (20:94).

وَقَفَّيۡنَا عَلٰٓى اٰثَارِهِمۡ بِعِيۡسَى ابۡنِ مَرۡيَمَ

Na Tukamfuatisha isa bin Mariamu katika nyayo zao, (5:47).

NB: Nabii Musa a.s. alipewa Taurati, lakini manabii wengi baada yake walihukumu kwa Taurati hiyo hiyo. Nabii Harun pia alikuwa chini ya amri ya Nabii Musa.

قَالَ اِنِّىۡ عَبۡدُ اللّٰهِ اٰتٰنِىَ الۡكِتٰبَ وَجَعَلَنِىۡ نَبِيًّا
وَّجَعَلَنِىۡ مُبٰرَكًا اَيۡنَ مَا كُنۡتُ

Akasema: hakika mimi ni Mtumishi wa Mwenyezi Mungu; Amenipa Kitabu na Amenifanya Nabii.

Na Amenifanya mbarikiwa popote nilipo. (19:31-32).

**Mwenyezi Mungu yupo kila mahali**

هُوَ اللّٰهُ فِى السَّمٰوٰتِ وَفِى الْاَرْضِ

Na yeye ndiye Mwenyezi Mungu katika mbingu na katika ardhi. (6:4).

فَاَيْنَمَا تُوَلُّوا فَثَمَّ وَجْهُ اللّٰهُ

Basi mahali popote mgeukiapo (mtaukuta) uso wa Mwenyezi Mungu. (2:116).

اَللّٰهُ نُوْرُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ

Mwenyezi Mungu ni nuru ya mbingu na ardhi (24:36).

**Ndoa na ahlul-Kitaab ni sahihi**

(Almaida:6).

**Ndoa na mshirikina imekatazwa**

(Al-Baqara:222).

**Nuzuul**

وَاَنْزَلَ لَكُمْ مِّنَ الْاَنْعَامِ ثَمٰنِيَةَ اَزْوَاجٍ

Mwenyezi Mungu amewateremshieni wanyama wanane (39:7).

قَدْ اَنْزَلَ اللّٰهُ اِلَيْكُمْ ذِكْرًا

رَّسُوْلًا يَّتْلُوْ عَلَيْكُمْ اٰيٰتِ اللّٰهِ مُبَيِّنٰتٍ

Mwenyezi Mungu amewateremshieni ukumbusho; Mtume anayewasomeeni aya za Mwenyezi Mungu zinazobainisha (65:11-12).

وَاَنْزَلْنَا الْحَدِيْدَ

Tukakiteremsha Chuma (57:26).

يٰبَنِيْٓ اٰدَمَ قَدْ اَنْزَلْنَا عَلَيْكُمْ

لِبَاسًا يُّوَارِيْ سَوْاٰتِكُمْ وَرِيْشًا

Enyi wanadamu hakika tumewataremshieni nguo zifichazo aibu zenu na mapambo (7:27).

**Nabii na Rasuul**

وَذْكُرْ فِى الْكِتٰبِ مُوْسٰٓى
اِنَّهٗ كَانَ مُخْلَصًا وَّكَانَ رَسُوْلًا نَّبِيًّا

Na umkumbuke Musa katika Kitabu, hakika yeye alikuwa mteule, na alikuwa Mtume, Nabii. (19:52).

وَذْكُرْ فِى الْكِتٰبِ اِسْمٰعِيْلَ اِنَّهٗ كَانَ
صَادِقَ الْوَعْدِ وَكَانَ رَسُوْلًا نَّبِيًّا

Na umkumbuke katika Kitabu Ismail, bila shaka yeye alikuwa mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii. (19:55).

وَمَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوْلٌ

Na siye Muhammad ila ni Mtume. (3:145).

مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (48:30).

يَآاَيُّهَا النَّبِىُّ

Ewe Nabii! (33:29, 46, 51, 60).

فَاٰمِنُوْ بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهِ النَّبِىِّ الْاُمِّىِّ

Basi Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, aliye Nabii Ummi, (7:159).

مَاالْمَسِيْحُ ابْنِ مَرْيَمَ اِلَّا رَسُوْلٌ

Masihi bin Mariamu siye ila ni Mtume tu. (5:76).

قَالَ اِنِّىْ عَبْدُ اللّٰهِ اٰتٰنِىَ الْكِتٰبَ وَجَعَلَنِىْ نَبِيًّا

Akasema hakika mimi ni mtumishi wa Mwenyezi Mungu; Amenipa Kitabu na amenifanya Nabii. (19:31).

**MERAAJ NA ISRAA NI SAFARI ZA KIROHO**

Ilikuwa hali ya ufunuo. 1.

فَاَوْحٰىٓ اِلٰى عَبْدِهٖ مَآاَوْحٰى

Na Akamfunulia mtumishi wake aliyomfunulia (53:11)

Ilikuwa safari ya kiroho 2.

مَاكَذَبَ الْفُؤَادُ مَا رَاٰى

Moyo haukusema uwongo uliyoyaona 53:12)

Ilikuwa njozi 3.

وَمَا جَعَلْنَا الرُّءْيَا الَّتِىٓ اَرَيْنٰكَ اِلَّا فِتْنَةً لِّلنَّاسِ

Na hatukuifanya njozi ile tuliyokuonesha ila kwa kuwajaribu watu (17:61).

Kufika mbinguni si katika uwezo wa watu 4.

قُلْ سُبْحَانَ رَبِّىْ هَلْ كُنْتُ اِلَّا بَشَرًا رَّسُوْلًا

Sema: Mola wangu ni Mtakatifu, mimi siye ila ni mtu tu, Mtume (17:94).

Bi Aisha anasema ilikuwa safari ya kiroho

"Wallah haukupotea mwili wa Mtume s.a.w. bali alipaa kwa kiroho (*Tafsir Kash shaaf* uk. 785).

Hadhrat Muawiyya r.a. anasema kwamba ilikuwa njozi ya 6. kweli. (*Durri Manthur* Jl. 4 uk. 197).

Hadhrat Hassab Basri amesema kwamba:

Ilikuwa njozi katika hali ya usingizi (*Tafsiri Kash Shaaf* uk. 758).

8. Mtume s.a.w. alilala katika Kaaba (Sahih Bukhari Kitaabu utauhid).

Kisha akaamka usingizini na hali yu katika Kaaba (*Sahihi* 9. *Bukhari Kitaabu Utauhid*).

Kifua na moyo wa Mtume s.a.w. ulisafishwa, kisha imani na 10. hekima zilijazwa ndani yake" (*Sahihi Bukhari, Baabul Miiraj).*

Usiku wa Miiraj Mtume s.a.w. aliingia Peponi. (*Sahihi* 11. *Bukhar Kitaabus Salaat).*

Qur'an Tukufu inasema kwamba wale ambao wanaingia peponi hawatolewi humo. (15:49).

Usiku wa Meeraj Mtume s.a..w alionyeshwa mito miwili Nile ya Misri na Farat ya Iraq.

Watu wa Makka walikadhibisha safari na walimwuliza 13. baadhi ya vitu lakini hakuweza kuwaeleza mpaka alionyeshwa tena saa ile ile na kawaelezea. *(Sahih Bukhari Kitabul Israa).*

Mtume Mtukufu s.a.w. alipewa maziwa, maji na pombe 14. alichagua maziwa.

Malaika Jibril alisema umechaguwa kitu sahihi kama

ungechagua maji au pombe ungepotea wewe na umati wako pia. (Ibne Jarir Jl. 15 uk. 6).

Mtume Mtukufu s.a.w. alionyeshwa mwanamke mkongwe. Malaika Jabril alimwambia kwamba huyo ni Dunia. (Ibne Jarir Jl. 15 uk. 6).

# BIBLIA

**Isa na Yesu**
**Sifa za Mungu**
**Mungu ni Mmoja**
**Yesu si Mungu**
**Kufufua wafu**
**Wana wa Mungu**
**Ukoo wa Yesu**
**Yesu mwana wa Adamu**
**Mke wa Yesu (Mariam Magdalene)**
**Yesu Mtume wa Mungu**
**Lengo la kutumwa Yesu**
**Lunga ya Yesu**
**Wanafunzi wa Yesu**
**Kazi za Yesu**
**Mizani ya imani ya Wakristo**
**Yesu kwa Waisraeli tu**
**Tabiri za Nabii Isa a.s.**
**Kafara ya Yesu**
**Yesu hakufa Msalabani**
**Watu wema kabla ya Yesu**
**Wahalifu wa Yesu (Anti Christ).**
**Mwana Mkuu wa Ibrahimu**
**Kupingana kwa Biblia**
**Maongezeko katika Biblia**

**Aya za Biblia zilizofutwa**
**Mtume Muhammad s.a.w. katika Biblia**
**Ujaji wa Yesu mara ya Pili**
**Marejeo Mbalimbali**
**Udhu na kuvua viatu**
**Ibada na Sala na saumu na Iddi**
**Nyimbo hazitakiwi**
**Masanamu hayatakiwi**
**Biblia na Wanawake**
**Biblia inaruhusu wake wengi**
**Nguruwe na Pombe ni haramu**
**Kutahiriwa**
**Yesu hakuzaliwa Dec. 25**
**Mwanzilishi wa Ukristo**
**Kumbuka kwa urahisi.**

## ISA NA YESU

**(Kutoka maandishi ya Sayyidna Ahmad a.s.)**

Tunamwamini na tunamheshimu Masihi wa kweli na mtakatifu ambaye hakudai kuwa mungu au mwana wa mungu na alitabiri ujaji wa Mtume Muhammad s.a.w. (Fathe-e-Masih uk. 13).

Ni jukumu langu kuthibitisha kwamba Isa a.s. alikuwa nabii mkweli na Mtakatifu wa Mwenyezi Mungu (Ayyam-us-Sulh uk. 2).

Mimi ni mfano wa Isa a.s. kwa hiyo siwezi kumwita mbaya. (Tabligh-e- Risalat uk. 70).

Hatumtambui Yesu ambaye alidai kuwa mungu na akawaita wa kabla yake kuwa wezi na wa baadaye waongo. (Anjam-e-Atham uk. 9).

Mapadre kwa kumtusi Mpendwa wetu Mtume Muhammad s.a.w. wametulazimisha kueleza hali kidogo ya Yesu na vitendo vyake (sawa na alivyoelezwa katika Biblia). Kama mapadre watubu na waahidi kwamba hawatamtusi Mtume Muhammad s.a.w., sisi pia hatutadhihirisha hali na siri zao waila litakuwa jiwe kwa jiwe. (Anjam-e-Atham uk. 8).

## SIFA ZA MUNGU

(Yakobo 1:13). Mungu hajaribiwi na Shetani. 1.
(Mat 4:1). Lakini Yesu alijaribiwa na Iblisi.

Mungu hafi (Daniel 6:26). 2.

Lakini Yesu alikufa sawa na Biblia.  (Mat. 27:50).

(1Wafalme 8:39)  Mungu anajua kila kitu.  3.
Lakini Yesu hakujua kila kitu (mti wa mtini).
(Mat. 21:18-19).
Ilhali haukuwa msimu wa matunda.
(Marko 11:13).

(Isaya 40:28).  Mungu hachoki.  4.
(Yoh. 4:6).  Lakini Yesu alichoka.

(Ezekiel 28:8-9).  Mungu hauwawi.  5.
(Matendo 5:30).  Lakini Yesu aliuwawa.

(Zaburi 121:3-4).  Mungu hasinzii.  6.
Lakini Yesu alilala fofofo.
(Marko 4:37-38; Mat. 8:23-25).

Mungu hali, lakini Yesu aliona njaa na akala.  7.
(Marko 11:12;  Luka 11:37-38, 24:42-43).
NB. Bwana Yesu Kristo hana sifa ya uungu hata moja.

## MUNGU NI MMOJA

1. Wewe naam, wewe - peke yako ndiye Mungu wa Falme zote za dunia; wewe ndiwe uliyeziumba mbingu na  nchi  (2 Wafalme  19:15).

2. Kwa kuwa ndiwe Uliye Mkuu wewe ndiwe Mfanya miujiza, ndiwe Mungu peke yako (Zaburi 86:10).

3. Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo
(Yohana 17:3). uliyemtuma.

4. ...... Na utukufu ule utakao kwa Mungu aliye wa pekee hamwutafuti? (Yohana 5:44).

5. Hakuna Mungu ila mmoja tu baki ni wa uwongo.
(1 Wakorintho 8:4-6).

6. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu?
(Marko 2:7).

7. Kumb. 6:4; 4:39. Nehemia 9:6. Isaya 43:10-11; 44:6; 44:8; 45:5; 45:21-22; 46:9. Marko 12:32. Luka 18:19; Mathayo 4:10; Warumi 3:30. Timotheo 1:17; 2:5.

## YESU SI MUNGU

*Naye Neno alikuwako kwa Mungu (Yohana 1:1).*

1. ... kama wewe na mimi ni umoja ulivyo ndani yangu nami ndani yako hao nao wawe ndani yetu ....... ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja.
(Yohana 17:21-23).

2. Mungu mmoja naye ni baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote (Waefeso 4:6).

3. Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu. (Yohana 14:20).

4. Suleiman anasema kwamba: Mimi nilikuwepo pamoja na Mungu hata kabla ya kuumbwa ardhi na mbingu. (Methali 8:22-30).

5. ... Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu. (Yohana 20:17).

6. Hakuna Mungu ila mmoja tu. kwa maana ijapokuwa wako waitwao miungu, ama mbinguni ama duniani, kama vile walivyoko miungu mingi na mabwana wengi; lakini kwetu sisi mungu ni mmoja tu, aliye baba, ambaye vitu vyote vinatoka kwake,
nasi tunaishi kwake. (1 Kor. 8:4-6)

7. Melkizedek mfalme wa Salem hana wazazi, hana mwanzo wala mwisho. (Waebrania 7:3).

8. Bwana akamwambia Musa angalia, nimekufanya wewe kuwa kama mungu kwa Farao na huyo ndugu yako Haruni atakuwa nabii wako. (Kutoka 7:1).

## YESU MWANA WA ADAMU

1. Mwana wa Adamu alikuja na kula na kunywa. (Mat. 11:19).

2. ........ Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi. (Mat. 12:40).

NB. Bwana Yesu Kristo katika Biblia mara nyingi sana ametajwa kama mwana wa Adamu.

3. Mat. 17:22; 9:6; 8:20; 16:27; 26:45; 12:40; 14:28
4. Marko 2:10; 9:31; 24:30; 26:45; 14:21-40
5. Luka 9:44.
6. Yohana 5:27
7. Matendo 7:56.

## WANA WA MUNGU

1. Bwana asema hivi, Israeli ni mwanangu mimi, mzaliwa wa kwanza wangu. (Kutoka 4:22).

2. Daudi ni mwana wa Mungu, yeye pia ni mwana wa kwanza. (Zaburi 89:26-27).

3. ....... Maana mimi ni baba wa Israeli na Efraimu (Ibrahimu) ni mzaliwa wa kwanza wangu. (Yeremia 31:9).

4. Sulaimani ni mwana wa Mungu.
(1 Mambo ya Nyakati 22:9-10).

5. ..... Mimi nimesema ninyi miungu.
(Yohana 10:34).

6. Wapatanishao wameitwa wana wa Mungu.
(Mat. 5:9).

7. Hata baada ya siku zile mkewe Elizabeti alichukua mimba akatawa miezi mitano, akisema, Hivi ndivyo alivyonitendea Bwana katika siku zile alizoniangalia ili kuniondolea aibu yangu mbele ya watu. (Luka 1:24-25).

## KUFUFUA WAFU

1. Elisha alifufua mtoto aliyefariki. (2 Wafalme 4:35).

Maiti alifufuka kwa kugusa mifupa ya Elisha. 2.
(2 Wafalme 13:21).
3. Ezekieli alifufua jeshi kubwa. (Ezekieli 37:10).

## UKOO WA YESU

1. Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahim. (Mathayo 1:1)

2. Salmon akamzaa Boazi kwa Rahabu*

(Mathayo 1:5)
* RAHABU alikuwa KAHABA (Yoshua 2:1)

3. Yuda akamzaa Peresi na Zera kwa Tamari*
(Mathayo 1:3)

*TAMARI alikuwa kahaba na mzinifu.
(Mwanzo 38:13-18)

4. Daudi alimzaa Sulemani kwa yule mke wa URIA.
(Mathayo 1:6)
Bath-Sheba mkewe URIA alipata mimba ya zinaa.
(2 Samuel 11:2-5)
Hawa mabibi wote wa Yesu walikuwa MAKAHABA NA WAZINIFU.
Biblia inasema kwamba "Mwana wa haramu asiingie katika mkutano wa BWANA; hata kizazi cha kumi asiingie aliye wake katika mkutano wa BWANA. (Kumbukumbu la Torati 23: 2).

**QUR`AN:** (A). Masihi bin Mariamu siye ila ni Mtume tu. Bila shaka Mitume wote wamekwisha fariki kabla yake, na mamake ni mwanamke mkweli.
(Qur`an 5:76).
(B). (Ewe Mariam) baba yako hakuwa mtu m`baya wala mama yako hakuwa asherati (Qur`an 19:29)

# MKE WA YESU (MARIYAMU MAGDALENA)

" Na bila shaka Tuliwatuma Mitume kabla yako, na Tukawapa wake na watoto. (Qur`an 13:39)

1. " Na tazama, mwanamke mmoja wa mji ule, aliyekuwa mwenye dhambi, alipopata habari ya kuwa ameketi chakulani katika nyumba ya yule Farisayo, alileta chupa ya marimari yenye marhamu. Akasimama nyuma karibu na miguu yake, akilia, akaanza kumdondoshea miguu machozi yake, na kupangusa kwa nywele za kichwa chake, akiibusu-busu miguu yake na kuipaka yale marhamu. Basi yule Farisayo aliyemwalika alipoona vile, aliseme moyoni mwake, Mtu huyu kama angekuwa nabii, angemtambua mwanamke huyu amgusaye, ni nani , na ni wa namna gani , ya kwamba ni mwenye dhambi." (Luka 7:37-39).

2. "Basi mtu mmoja alikuwa hawezi Lazaro wa Bethania, mwenyeji wa mji wa Mariamu, dada yake. Ndiye Mariamu yule aliyempaka Bwana marhamu, akamfuta miguu kwa nywele zake, ambaye Lazaro nduguye alikuwa hawezi. (Yohana 11:1-2).

3. "Basi Mariamu akatwaa ratili ya marhamu ya nardo safi yenye thamani nyingi, akampaka Yesu miguu, akamfuta miguu kwa nywele zake." (Yohana 12:3).

4. "Akamgeukia yule mwanamke, akamwambia Simon.

Wamwona mwanamke huyu? Niliingia nyumbani kwako, hukunipa maji kwa miguu yangu; bali huyu amenidondoshea machozi miguu yangu, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake. Wewe hukunibusu; lakini huyu tangu nilipoingia hakuacha kunibusu sana miguu yangu. Hukunipaka kichwa changu mafuta; bali huyu amenipaka miguu yangu marhamu." (Luka 7:44-46).

5. " Basi Mariamu ali pofika pale alipokuwapo Yesu, na kumuona, alianguka miguuni pake, akamwambia, Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa. Basi Yesu alipomuona analia na wale Wayahudi waliofuatana naye wanalia, aliugua rohoni, akafadhaika roho yake, akasema mmemweka wapi? Wakamwambia, Bwana, njoo utazame. Yesu akalia machozi." (Yohana 11: 32-35).

7. Bwana harusi (Yesu Kristo) alitengeneza divai nzuri sana. (Yohana 2:1-10).

## YESU, MTUME WA MUNGU

1. Yesu ni mtume (Qur`an 4:172, 5:76, 61:7

2. Akajibu, akasema sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.
( Mathayo 15:24)

3. Na uzima wa milele ndio huu, wakujuwe wewe,

Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma. (Yohana 17:3)

... bali yeye ndiye aliyenituma. (Yohana 8:42). 4.

... Baba aliyenipeleka. (Yohana 14:24) 5.

... Wewe ndiye uliyenituma. 6.
(Yohana 17: 8-14,21-22).

Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama 7.
nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo; na hukumu yangu ni ya haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka.
(Yohana 5:30, 6:38, 4:36).
**Mathayo** 21;46 - 21:11, 9:37. **Mk.** 9:35;
**Luka** 4:43-24:19, **Yohana** 13:20, 12:44-50, 7:16-17, 6:57 - 6:44, 7:28-29-33, 8:16-18-26-29, 9:4, 9:17,6:14, 15:22; 16:5, 17:17:21-23-25, 4:19-24-44

## YESU ALITUMWA KWA WANA WA ISRAELI TU

1. Alisema, sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. (Mat. 15:24).

2. Akasema si vema kukitwaa chakula cha watoto na

kuwatupia mbwa. (Mat. 15:26; Marko 7:27).

3. Msishike njia kuyaendea mataifa. (Mat:10:5-6).

4. Yesu anawaambia wanafunzi wake hawataimaliza miji ya Israeli kabla ya kurudi kwake.
(Mat:10-23).

5. Wanafunzi wa Yesu walimpinga Petro kwa sababu ya kuihubiri Injili kwa Mataifa.
(Matendo 11:1-3).
6. Paulo alichukizwa kwa sababu ya kukataliwa na Mayahudi, hivyo akaanza kuyahubiri Mataifa
(Matendo 18:5-6).
Mathayo 2:6; 2:2; 19:26. Luka 1:32-33; 22:29-30.
Matendo 13:23

7. Yesu Mfalme wa Wayahudi.
(Mat. 2:6; 27:29, 42; Yohana 1:49).

8. Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu.
(Luka 2:1).

NB. Kaisari alikuwa mfalme wa nchi ya Rumi. Neno ulimwengu lilimaanisha miji aliyoitawala tu. (Jibu la nendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi.
(Mat. 28:19).

# YESU ALILETA UPANGA

Bwana Yesu mwenyewe anatuelezea lengo la kutumwa kwake:

Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la, 1. sikuja kuleta amani, bali upanga. Kwa maana nalikuja kumfitiini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu.
(Mat 10:34-35).

2. Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.
(Luka 14:26).

3. Je, mwadhani ya kwamba nimekuja kuleta amani duniani? Nawaambia la, sivyo, bali mafarakano. (Luka 12:51).

4. Akawaambia "Lakini sasa mwenye mfuko na auchukue,na mwenye mkoba vivyo hivyo; naye asiye na upanga akauze joho lake akanunue.
(Luka 22:36)

5. Yesu akaingia ndani ya hekalu, akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni. Akazipindua meza za wabadili fedha, viti vyao walikuwa wakiuza njiwa. (Mathayo 21:12).

6. Akamwaga fedha za wenye kuvunja fedha, akazipindua meza zao. (Yohana 2:15).

7. Mwanafunzi alitumia upanga na kukata sikio. (Mathayo 26:51).

**Qur'an:** Nisadikishaye yaliyo mbele yangu katika Torati na kutoa habari njema ya Mtume atakayefika nyuma yangu jina lake ni Ahmad. (Qur'an 61:7).

## LUGHA YA YESU

Wasioamini (wasio Waisraeli) wameitwa mbwa na 1 nguruwe. (Mathayo 7:6).

Aliwaita watu wabaya "Enyi wazao wa nyoka". 2. (Mathayo 12:34)

Mayahudi waliitwa "Kizazi cha zinaa." 3. (Mathayo 12:40, 16:4).
Mayahudi waliitwa " Wazinifu na wakosefu". 4. (Marko 8:38).

Ole wenu waandishi na wafarisayo, wanafiki. 5. (Mathayo 23:13.

Ole wenu viongozi vipofu. (Mathayo 23:16). 6

Enyi nyoka, wana wa majoka. (Mathayo 23:33). 7.

Watu wengine waliitwa mbwa. (Mathayo 15:27) 8.

Aliwaita manabii wezi "wote walionitangulia ni wevi na 9.
wanyang`anyi. (Yohana 10:8).

Aliwaita wanafunzi wake "Enyi kizazi kisicho amini, 10.
kilichopotoka, (Mathayo 17:17).

Akamwambia Petro "Nenda nyuma yangu Shetani.11.
(Mat 16:23).

Akamwambia mama yake " Ewe mwanamke nina 12.
nini nawe? (Yoh: 2:4)

Akasema mama yangu ni nani na ndugu zangu ni 13.
akina nani? (Mat: 12:48).
Siku ya Kiyama atawaita wahubiri 14.
Wakristo."Nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.
(Mathayo 7:23).

## WANAFUNZI WA YESU

Yesu alisema, Hata sasa ninyi nanyi mngali hamna 1.
(Mathayo 15:16). akili?

Alimwambia Petro kwamba:," Ewe mwenye imani 2.
haba, mbona uliona shaka? (Mathayo 14:31)

Petro alikanusha kuwa mfuasi wa Yesu mara tatu 3.
bali alimlaani. (Mathayo 26:69-75).

Yuda Iskariote alimuuza Yesu kwa shilingi 30 tu. 4.
(Mathayo 26:15).

Wakati Yesu alikuwa hatarini, wanafunzi waliendelea 5.
kulala (mathayo 26:40-45; Mk. 14:36-41).
(Mathayo 27:5). Yuda alijinyonga. 6.

Imani ya wanafunzi - " kwa sababu ya upungufu wa 7.
imani yenu. " (Mathayo 17:20).

Ndipo wanafunzi wote wakamwacha wakakimbia. 8.
(Mathayo 26:50).
Wengi wataniambia siku ile; Bwana, Bwana, 9.
hatukufanya unabii kwa jina lako, kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.
(Mathayo 7:22-23).

**QUR'AN:** Enyi mlioamini! Muwe wasaidizi wangu kwa Mwenyezi Mungu. Kama alivyosema Isa bin Mariam kuwaambia wanafunzi (wake): Ni nani wasaidizi wangu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu? Wanafunzi wakasema: Sisi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu.
(Qur’an 61:15).

## MIUJIZA YA YESU KRISTO
## WAKRISTO WAONESHE MIFANO HII!

Kuponya wagonjwa. 1.
(Mathayo 8:16, 9:22, Na 15:21).

Kuponya walemavu. (Mathayo 8:1-3). 2.

Kuponya mabubu. (Mathayo 9:3-7; 12-22). 3.
Kuponya mwenye kupooza upande mmoja. 4.
(Mathayo 8:5-13. 9:1-7, 12:22).

Kumponya mwenye kifafa. (Mathayo 17:14-19). 5.

Kuponya mkono wenye ukoma. 6.
(Mathayo 12:15)

Kuponya mgongo uliopinda. (Luka 13:10). 7.

Kuwafufua wafu (Mathayo 9:24). 8.

Kugeuza maji kuwa pombe (Yohana 2:1-9) 9.

Chakula kidogo kitoshe watu elfu tano. 10.
(Mathayo 14:13-21)
Kutembea juu ya maji. (Mathayo 14: 22-33). 11.

Kuzuia tufani ya maji ya ziwa. 12.
(Mathayo 8:23-33)

# MIZANI YA IMANI YA WAKRISTO

Bwana Yesu Kristo alieleza mizani na alama za imani kama ifuatavyo:

1. Mkiwa na imani kiasi ya punje ya haridari, mtauwambia mlima huu, ondoka hapa nenda kule, nao utaondoka; wala halitakuwapo neno lisilowezekana kwenu. (Mathayo 17:20, 21:21; Mk. 11:22-23, 9:23; Lk. 17:6, 12-13:2).

2. Bwana akasema: " kama mngekua na imani kiasi cha chembe ya haridari mngeuwambia mkuyu huu, ng`oka, ukapandwe baharini, nao ungewatii.
(Luka 17:6)

3. Yesu akajibu, akawaambia, Amin, nawaambia mkiwa na imani, msipokuwa na shaka, mtafanya si hilo la mtini tu, lakini hata mkiwambia mlima huu,ng`oka ukatupwe baharini, litatendeka. Na yeyote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea. (Mathayo 21:21-22)

4. Amin, Amin, nawambieni, Yeye aniamiaye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya ili baba atukuzwe ndani ya mwana".
(Yohana 14:12-13).

5. Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. (Yohana 15:7).

6. Tena nawaambia, ya wawili wenu matakapopatana duniani katika jambo lolote watakalo liomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. (Mathayo 18:19)

7. Ombeni nanyi mtapewa ... (Mathayo 7:3-12)
**TAMBIO:** Tunawapa Wakristo tambio (challenge) kwamba kama wanayo imani sawa na chembe ya haridali, watuoneshe miujiza iliyotajwa hapo juu. Mkristo mmoja au wawili au wajumuike wote, sisi tunataka kuona miujiza ya imani yao.

## ANTI CHRIST/ WAHALIFU WA YESU

**Paulo ni mhalifu wa Yesu.**
Yesu Alisema:
1. Katika njia ya Mataifa msiende. (Mathayo 10:5)
Lakini Paulo akafundisha:
A. Nimekabidhiwa Injili ya wasiotahiriwa (Wagalatia 2:7, maandishi ya Paulo).
B. Amewafungulia mataifa mlango wa imani (Matendo ya Mitume 14:27, ya Paulo).

2. Yesu alitahiriwa. (Luka 2: 21).
Lakini Paulo alipinga kutahiriwa (Matendo ya Mitume 21:21).

Yesu Alisema:

3. Msidhani kuwa nalikuja kuitangua Torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie. Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni. Maana nawaambia ya kwamba, Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kwamwe katika ufalme wa mbinguni. (Mathayo 5:17-20).

Lakini Paulo anasema:

Sheria ni laana.

(Wagalatia 2:16-21, 3:10-13, (Warumi 7: Yote)

Bwana Yesu alisema: 4.

Msichukuwe dhahabu, wala fedha, wala mapesa mifukoni mwenu; (Mathayo 10:9).

Hivyo Wakristo wale ambao wanakusanya mali ni Madajjali (Anti Christ).

Bwana Yesu alisema: 5.
Lakini mimi nawaambia msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigae shavu la kuume mgeuzie na pili. Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia.
(Mathayo 5:39-40).
Hivyo Wakristo wale ambao wanagombana ni Madajjal (Anti Christ).
Yesu pia alikataza kuitwa Kristo: 6.
Ndipo alipowakataza wanafunzi wake wasimwambie mtu yeyote kwamba yeye ndiye Kristo.
(Mathayo 16:20)
Hivyo Wakristo ambao wanatangaza kwamba Yesu ndiye Kristo ni Madajjal (Anti Christ).

Bwana Yesu alisema: 7.
Kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe. (Mathayo10:35); Luka 14:26, 12:51-52).
Hivyo Wakristo ambao wanapenda amani wala hawatumii upanga ni Madajjal (Anti Christ).

## YESU HAKUFA MSALABANI

1. Aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu.
(Kum. 21:23, Wagalatia 3:13.

Lakini Yesu alikuwa nabii wa Mwenyezi Mungu, hivyo hawezi kuwa mlaaniwa.

2. Wafu hawawezi kurejea duniani (Ayubu 7:9).

3. Ishara ya Nabii Yona, yaani wakati alipoingia, siku tatu alizokaa na alipotoka ndani ya tumbo la nyangumi, nyakati zote alikuwa hai. (Mat. 12:39-40).

4. Damu ilibubujika mara tu alipochomwa mkuki na askari baada ya kutangazwa kuwa amekufa.
(Yohana 19:34).

5. Yesu pia alijificha kwa kuhofia asikamatwe.
(Yohana 11:53-54; 12;36).

6. Yesu alikutana na wanafunzi wake Galilaya. wanafunzi walipodhani kwamba huyu ni roho wa Yesu, bwana Yesu aliwaonyesha mwili wake na majeraha yake na akala mbele yao na kusema kwamba roho haina mwili wala mifupa.
(Luka 24:39).
7. Yesu akaenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi akaomba akisema; Baba yangu ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke walakini si kama nitakavyo mimi bali kama utakavyo wewe (Mathayo 26:39).
NB. Maombi ya Bwana Yesu yalikubaliwa na Mungu.
Yeye katika siku hizo za mwili wake alimtolea yule a) aliyeweza kumuokoa na kumtoa katika mauti maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi akasikilizwa kwa

jinsi alivyokuwa mchamungu (Waebrania 5:7).
Akasema baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia b)
nami nilijua ya kuwa wewe wanisikia siku zote (Yohana
11:41-42).

Pilato alitaka kumwachia Yesu (Luka 23:20; Mat 8.
27:22; Marko 15:9; Matendo 3:13; Yohana 18:38-40,
19:14-15).
Pilato alishangaa alipoambiwa kwamba Yesu alikuwa -
amekufa (Marko 15:44).
Yesu alikuwa na uhakika kwamba maombi yake -
yamekubaliwa na ndio maana alipoona hali imekuwa
mbaya zaidi hata kinyume cha matarajio yake
akashangaa kwa kusema: Eloi, Eloi, lama sabakthani?
Yaani Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?
(Mat 27:46; Marko 15:34).

9. Na kondoo wengine ninao ambao si wa zizi hili, na hao
nao imenipasa kuwaleta na sauti yangu wataisikia kisha
kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja. (Yohana
10:16).
10. Ndoto ya mke wa Pilato. (Mat 27:19)
11. Jiwe mlangoni pa kaburi (Mat 27:60; Marko 15:46).

Basi ikiwa Kristo anahubiriwa ya kwamba amefufuka 12.
katika wafu, mbona baadhi yenu husema kwamba
hakuna kiyama ya wafu? Lakini kama hakuna kiyama ya
wafu, Kristo naye hakufufuka. Tena kama Kristo

hakufufuka, basi, kuhubiri kwetu ni bure na imani yenu ni bure. Naam, na sisi tumeonekana kuwa mashahidi wa uwongo wa Mungu. Kwa maana tulimshuhudia Mungu ya kuwa alimfufua Kristo, ambaye hakumfufua, ikiwa wafu hawafufuliwi. Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure. Mngalimo katika dhambi zenu. Na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea. Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi tu maskini kuliko watu wote. (1 Wakorintho 15:12-19).

## **KAFARA YA YESU HAISAIDII**

1. ... Nataka rehema wala si sadaka. (Mat. 12:7). Mungu husamehe kutokana na maombi ya Nabii. (Kumb. 9:18-20).

2. Mkiwasamehe watu makosa yao nanyi mtasamehewa na baba yenu aliye mbinguni.
(Mat. 6:14).

3. Kabla ya kafara ya Yesu walipatikana watakatifu wasio na dhambi. (Melkizedeki (Waebrania 7:3), Yohana Mbatizaji (Luka 1:15), Zakaria na Elizabeth (Luka 1:6).

4. Yesu hakutaka afe msalabani. (Mat. 27:46).

5. Yesu anakataa kuitwa mwema.
Hakuna aliye mwema ila mmoja ndiye Mungu.
(Marko 10;18).

6. Azaliwaye na mwanamke si safi. (Ayubu 25:4).

Mwanamke ndiye aliyekula tunda kwanza.
(Mwanzo 3:6).

7. Yesu hakutuokoa na dhambi ya asili kwani adhabu zilizotolewa kwa sababu ya kosa hilo la Adamu na Hawa bado zinaendelea kuwepo hata baada ya kafara yake.
(Mwanzo 3:14-19).

8. Wazo la kafara halikubaliwi na Mungu.
(Kutoka 32:30-33).

9. Mababa wasiuwawe kwa ajili ya watoto wao, wala watoto wasiuwawe kwa ajili ya baba zao; kila mtu na auwawe kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe.
(Kumb. 24:16).

10. Lakini kila mtu aipime kazi yake mwenyewe, ndipo atakapokuwa na sababu ya kujisifu ndani ya nafsi yake tu; wala si kwa mwenzake.
(Wagalatia 6:4).

11. Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe.

(Wagalatia 6:5).

## WATU WEMA KABLA YA YESU

Henoko aliienda pamoja na Mungu. 1.
(Mwanzo 5:22-24).

Zakaria na mkewe, wote wawili walikuwa wenye haki 2.
mbele za Mungu, wakienda katika amri zote za Bwana na maagizo yake bila lawama. (Luka 1:5-6).
**Swali:** Iwapo watu hao wote na wengineo walikuwa wema na wasio na lawama mbele ya Mungu, walipataje uwokovu wakati Yesu alikuwa hajafika?

## MWANA MKUU WA IBRAHIM

**ABRAHAM MUME WA HAGAR**
Sarai, mkewe Abraham akamtwaa Hajira Mmisiri mjakazi wake baada ya kukaa Abraham katika nchi ya Kanaan miaka kumi akampa Abraham mumewe awe mkewe. (Mwanzo 16:3).

## ISMAIL MWANA ALIYEAHIDIWA

"Malaika wa Bwana akamwambia: Hakika nitauzidisha uzao wako, wala hautahesabika kwa jinsi utakavyo kuwa mwingi. Malaika wa Bwana akamwambia: Tazama

wewe una mimba utazaa mwana wa kiume nawe utamwita jina lake Ishmaeli maana Bwana amesikia kilio cha mateso yako."
(Mwanzo 16:10-11)

## ISMAIL MWENYE BARAKA

Na kwa habari za Ishmael nimekusikia, Nime`mbariki, nitamzidisha nami nitamwongeza sana sana. Atazaa Masayid kumi na wawili nami nitamfanya awe Taifa kuu. (Mwanzo 17:20).

**ISMAILI MWANA WA IBRAHIM** Sara akamwona yule mwana wa hajiri Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka. (Mwanzo 21:9).
Ibrahim akamtwaa Ismaeli mwanawe.
(Mwanzo 17:23)

## MWANA MKUU WA IBRAHIM

(A). Naye Ibrahimu alikuwa mtu wa miaka 86, hapo Hajira alipomzalia Abrahamu Ismaeli.
(Mwanzo 16:16)
(B). Naye Ibrahim alikuwa mtu wa miaka mia alipozaliwa mwana wake Isaka. (Mwanzo 21:5).

## MUNGU ALIMSIKIA ISMAIL NA ALIM'BARIKI

Mungu alisikia sauti ya kijana, Malaika wa Mungu akamwita Hajira kutoka mbinguni, akamwambia Hajira! Usiogope maana Mungu amesikia sauti ya kijana huko aliko. "Ondoka ukamwinue kijana ukamshike mkononi mwako kwa kuwa nitamfanya kuwa Taifa kubwa. (Mwanzo 21:17-18).

## MUNGU PAMOJA NA ISMAIL

Mungu akawa pamoja na huyo kijana naye akakua, akakaa katika Jangwa akawa mpiga upinde.
Akakaa katika Jangwa la Parani mama yake akamtwalia mke katika nchi ya Misri,
(Mwanzo 21:20-21)

## KUPINGANA KWA MAANDIKO YA BIBLIA

1. Mwanadamu aliumbwa baada ya uumbaji wa wanyama. (Mwanzo 1:25-26).
Lakini katika (Mwanzo 2:18-20), inaonekana mwanadamu aliumbwa kwanza.

2. Mwandishi wa Torati siye Nabii Musa mwenyewe.
Basi Musa mtumishi wa bwana akafa huko katika nchi ya Moabu kwa neno la Bwana. (Kumb. 34:5).

3. Yesu alifyolewa na wanyang’anyi wawili aliposulubiwa pamoja nao.
(Marko 15:32 ; Mat. 27:44).
Lakini katika Luka 23:39-40, inasema kuwa mnyang’anyi mmoja ndiye aliyemfyolea Yesu.
4. Yuda alijinyonga. (Mat. 27:5).
Lakini katika Matendo 1:18, imeandikwa kwamba alianguka na kupasuka matumbo yake.

5. Sungura hucheua (Mambo ya Walawi 11:6). Lakini ukweli ni kwamba Sungura hacheui kabisa.
6. Yuda aliyemsaliti Yesu alivitupa vile vipande vya fedha alivyopewa kwa udhalimu wake huo, kisha alijinyonga na wakuu wa Makuhani wakavichukua vipande vya fedha na wakanunulia shamba la
kuzikiwa watu (Mat 27:5-7).
Lakini (Matendo 1:18), inasema kwamba Yuda mwenyewe alinunua konde kwa ijara aliyoipata kwa udhalimu wake huo na kisha akaanguka na kupasuka na matumbo yake yote yakatoka.

7. Mwandishi wa Kitabu cha Mathayo si Mathayo mwenyewe ambaye ni mwanafunzi wa Yesu.
(Mat. 9:9).

8. Yehoremu alishikilia kutawala wakati akiwa na umri wa mika 32 alifariki katika miaka 40

(2 Mambo ya Nyakati 21:5)
(2 Mambo ya Nyakati 21:20).
Baada ya kifo chake mtoto wake mdogo alishikilia serikali na alikuwa na umri wa miaka 42 wakati ule.
(2 Mambo ya Nyakati (22:1-2).
Kana kwamba mwana mdogo alikuwa miaka miwili zaidi kuliko baba mzazi!
(9. Mat 5:17; Mat 5:38-40; Hebrew 7:12).

Harun alikufa huko Hor. (Hesabu 33:38)
Haruni alikufa huko Mosera (Kumb. 10:6)

Michael binti wa Saul hakupata mtoto mpaka kifo chake.
(2 samweli 6:23)
Michael binti wa Saul alikuwa na wavulana watano
(2 Samweli 21:8)
Benjamin alikuwa na watoto watatu.
(1 Mambo ya Nyakati 7:6)
Benjamin alikuwa na watoto watano.
(1 Mambo ya Nyakati 8:1-2.

## MAONGEZEKO KATIKA BIBLIA

Yaliyo siyo maneno ya Mungu wala ya Mitume

1. Kumb. 1:1-5; 34:5-12
Joshua 1:1; 24:29-33
Waamuzi: 1:1
Yohana 1:1; 21:25
Mat 9:9
Mambo ya Walawi 1:1; 27:34
Hesabu 1:1; 36:13
Mithali 1:1
Kumb. 1:1
Wimbo ulio bora 1:1
Isaya 1:1

## AYA ZA BIBLIA ZILIZOFUTWA

**Aya za Biblia zilizofutwa katika chapa mpya***
Mathayo: (12:47; 17:21; 18:11; 21:44; 23;14).

Zilizofutwa nusu ya pili. (6:13; 27:49).
Marko: (7:16; 9:44-46; 11:26; 15:28).
Luka: (17:36; 22:43-44; 23:17; 24:12; 24:40).
Yohana: (5:4; na 5:3 nusu ya pili).

*chapa mpya ya:

1. Revised standard Version.
2. The Good News Bible.
3. The Holy Bible.
4. The Bible James Version.
5. Biblia Habari Njema.

# TABIRI ZA YESU

Amini nawaambieni pana watu katika hawa 1.
wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa hata watakapomwona mwana wa adamu akija katika ufalme wake. (Mathayo 16:28).

Yesu akawaaambia, amini nawaaambia ya kwamba 2.
ninyi mlionifuata mimi katika ulimwengu mpya, Atakapoketi mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na mbili mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli (Mathayo 19:28).

Yuda alimuza Yesu kwa shilingi thelathini tu. (Mathayo 26:15).

Ewe Petro nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa 3.
mbinguni. (Mathayo 16:19).

Petro alikanusha kuwa mfuasi wa Yesu mara tatu bali alimlaani. (Mathayo 26: 69-75).

Mwizi aliyewambwa msalabani, Yesu akamwambia 4.
Amini nakuambia leo hivi utakuwa pamoja nami peponi. (Luka 23:43).

(Baada ya siku tatu alisema) Kwa maana sijapaa kwenda kwa baba. (Yohana 20:17).

## MTUME MUHAMMAD s.a.w.
## KATIKA BIBLIA

1. Mtume mfano wa Nabii Musa a.s. atakuja. (Kumb. 18:18-19).

a. Nabii yule hajaja. (Matendo 3:18-22).

b. .... lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli atawaongoza awatie kwenye kweli yote. (Yoh. 16:12-13).

2. Mlima Paran, watakatifu elfu kumi, na sheria motomoto. (Kumb. 33:2).

(a) Ismail akakaa katika jangwa la Paran na mama yake. (Mwanzo 21:21).

3. Ufalme wa Mungu utapewa watu wengine. (Mat. 21:43).

4. ... Hamtaniona kamwe tangu sasa hata mtakaposema amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana. (Mat. 23:39).

5. Muhammad s.w.a. ndiye Roho (Quran 58:33).

## UJAJI WA YESU MARA YA PILI

1. .. Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana. (Mat.

23:39).
Yesu pia anaitwa bwana katika Istilahi ya Biblia. (Matendo. 1:21; Warumi 4:24; 2Wakorintho 4:5, 13:14, 11;31; Wagalatia 1:3, 6:14, 6:18 1:17; Waefeso 1:15; 1:17, 6:23-24; 2Petro 1:2, 8, 16).

2. Eliya alipaa mbinguni (2 Wafalme 2;11).
Katika (Malaki 4:5) inasemwa kuwa Eliya atarudi, lakini katika (Mat. 11:14; 17:12), inasemwa kuwa Yohana Mbatizaji ndie Eliya.

3. Ujaji wa Yesu wa mara ya pili utakuwa sawa na ujaji wa mwizi.
(Mat. 24:43). (Ufunuo 3:3) na Petro 3:10).

4. Yesu atakuja kama umeme (Mathayo 24:27).

5. Kupatwa kwa jua na mwezi Mat. 24:29

6. Kutakuwa na vita na matetemeko na tauni na njaa kila mahali. (Luka 21:10-11).

Atakuja katika saa, watu wasiyoitegemea. 7.
(Mat 24:44).

8. Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakio na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue, hata

Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. (Mat 24:37-39).

## MAREJEO MBALIMBALI

### Udhu

Bwana akanena na Musa na kumwambia fanya na birika la shaba, na tako lake la shaba ili kuogea, nawe utaliweka kati ya hema ya kukutania na madhabahu nawe utalitia maji. Na Haruni na mwanawe wataosha mikono yao na miguu yao humo hapo waingiapo ndani ya hema ya kukutania, watajiosha majini ili wasife au hapo watakapoikaribia madhabahu ili watumike kumteketezea Bwana sadaka ya moto basi wataosha mikono yao na miguu yao ili kwamba wasife na neno hili litakua amri kwao milele kwake yeye na kwa wazao wake katika vizazi vyote.
(Kutoka 30:17-21).

Basi kulikuwako huko mabalasi sita ya mawe nayo yamewekwa huko kwa desturi ya Wayahudi ya kutawadha. Kila moja lapata kadiri ya nzio mbili tatu.
(Yohana 2:6).

## Kuvua viatu wakati wa ibada

Huyo Amiri wa jeshi la Bwana akamwambia Yoshua, vua viatu vyako miguuni mwako kwa kuwa mahali hapo usimamapo ni patakatifu, Yoshua akafanya hivyo. (Yoshua 5:15).

Naye akasema usikaribie hapa, vua viatu vyako miguuni mwako maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu. (Kutoka 3:5).

## Ibada na Sajda

Naye Ezra Kuhani akasimama juu ya mimbari ya mti waliyokuwa wameifanya kwa kusudi hilo na karibu naye akasimama Matithia ....... Ezra akakifungua kitabu machoni pa watu wote (maana alikuwa juu ya wote) na hapo alipokijua, watu wote walisimama Ezra akamhimidia Bwana, Mungu Mkuu. Nao wote wakaitika Amina, Amina, pamoja na kuinua mikono yao kisha wakainama vichwa vyao wakamsujudia Bwana vifudifudi. (Nehemia 8:4-12; Mwanzo 17:3).

Akaendelea mbele kidogo akaanguka kifulifuli akaomba ... (Mathayo 26;39).

Msujudie Mungu. (Ufunuo 22:9).

Musa akafanya haraka akainamisha kichwa chake hata nchi, akasujudu.
(Kutoka 34:8; 1 Wakorintho 14:25)

## Nyimbo Hazitakiwi

Niondoleeni kelele za nyimbo zenu; kwa maana sitaki kuzisikia sauti za vinanda vyenu. (Amosi 5:23).

Ninyi mnaoimba nyimbo za upuzi pamoja na sauti ya vinanda na kujifanyizia vinanda vya namna nyingi kama vile Daudi. (Amosi 6:5).

Tena nyimbo za hekaluni zitakuwa vilio siku ile, asema Bwana Mungu. Mizoga itakuwa mingi kila mahali wataitupa wakinyamaza kimya. (Amosi 8:3).

## Masanamu hayatakiwi

Usiwe na miungu mingine ila mimi.
Usijifanyie sanamu ya kuchonga, mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, au kilicho chini duniani, au kilicho majini chini ya nchi. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu, (Kumb. 5:7-9).

## Wanawake na wanaume wasichanganyike kwa maombolezi (ibada)

Nayo nchi itaomboleza kila jamaa peke yake; jamaa wa nyumba ya Daudi peke yao, na wake zao peke yao;

jamaa wa nyumba ya Nathani peke yao na wake zao peke yao; jamaa wa nyumba ya Lawi peke yao na wake zao peke yao; jamaa wa nyumba ya Shimri peke yao na wake zao peke yao. Jamaa zote zilizosalia, kila jamaa peke yao na wake zao
peke yao. (Zakaria 12:12-14).

## Wanawake wajipambe kwa kujisitiri.

Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi kwa kujisitiri, pamoja na adabu nzuri na moyo wa kiasi, si kwa kusuka nywele wala kwa dhahabu na
lulu kwa nguo za thamani. (1 Tim. 2:9-12).

Bali kila mwanamke asalipo au anapohutubu, bila kufunika kichwa yuaibisha kichwa chake kwa maana ni sawa na yule aliyenyolewa.
(1 Wakorintho. 11:5).

## Wanawake wasihubiri

Wanawake na wanyamaze katika kanisa maana hawana ruhusa kunena bali watii kama vile inenavyo Torati nayo. Nao wakitaka kujifunza neno lolote, nawawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao, maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa. (1 Wakorintho 14:34-35).
Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha wala kumtawala

mwanamume, bali awe katika utulivu.
(1 Timotheo 2:12).

## Mwanamke akiwa katika hedhi.

Mwanamke yeyote, kama anatokwa na kitu, na kitu chake alichokuwa nacho mwilini mwake ni damu, ataketi katika kutengwa kwake muda wa siku saba na mtu yeyote atakayemgusa atakuwa najisi hata jioni.
(Mambo ya Walawi 15:19).

## Biblia inaruhusu mitala (wake wengi)

Akiwa mtu ana wake wawili, mmoja ampenda, mmoja 1.
hampendi .... (Kumb. 21:15-17).
Nabii Ibrahim alikuwa na wake wawili 2.
(Mwanzo 16:1-4).

Nabii Daud alikuwa na wake wengi na masuria 3.
(2 Samuel 12:8 na 15:16).

Nabii Suleiman alikuwa na wake mia saba na masuria 4.
mia tatu. (1 Wafalme 11:3).

## Kuoga Janaba

Na mtu yeyote akitokwa na shahawa yake, ndipo ataoga mwili wake wote majini, naye atakuwa najisi hata jioni. Na

kila nguo na kila ngozi, ambayo ina shahawa itafuliwa kwa maji itakuwa najisi hata jioni. Huyo mwanamke naye ambaye mtu mume amelala naye kwa shahawa, wote wawili wataoga majini, nao watakuwa najisi hata jioni. (Mambo ya Walawi 15:16-18).

## Nguruwe ni haramu

Naye nguruwe kwa sababu yeye anazo kwato, ni mwenye miguu iliyopasuka kati lakini hacheui, yeye ni najisi kwenu. Msile nyama yao, wala msiiguse mizoga yao, hao ni najisi kwenu.
(Mambo ya Walawi 11:7-8).

Waketio kati ya makaburi, na kulala katika mahali pao pa siri, walao nyama ya nguruwe, na mchuzi wa vitu vinichukizavyo u katika vyombo vyao.
(Isaya 65:4). (Kumb. 14:8).

## Pombe ni haramu

Usiitazame mvinyo iwapo ni nyekundu, litiapo bilauri rangi yake ishukapo taratibu; mwisho wake huuma kama nyoka; Huchoma kama fira. Macho yako yatakuwa mambo mageni; na moyo wako utatoa yaliyopotoka, Naam, utakuwa kama alalaye katikati ya bahari; Au kama yeye asinziaye juu ya mlingoti. Utasema, wamenichapa wala sikuumia, wamenipiga wala sina

habari, Nitaamka lini, nitazidi kuitafuta tena.
(Mithali 23:31-35).
Wote ni mbwa walio bubu, hawawezi kulia, huota ndoto, hulala, hupenda usingizi. Naam, mbwa hao wana choyo sana, hawashibi kamwe; na hao ni wachungaji wasioweza kufahamu neno, wote pia wamegeuka upande, wazifuate njia zao wenyewe kila mmoja kwa faida yake toka pande zote. Husema, njooni nitaleta divai, na tunywe sana kileo na kesho itakuwa lama leo sikukuu kupita kiasi.
(Isaya 56:10-12).

Ole wao waamkao asubuhi na mapema, wapate kufuata kileo, wakishinda sana hata usiku wa manane mpaka mvinyo imewaka kama moto ndani yao! Na kinubi, na zeze na matari na filimbi, na mvinyo zote ziko katika karamu zao lakini hawaangalii kazi ya Bwana wala kuyafikiri matendo ya mikono yake.
(Isaya 5:11-12).

Ole wao walio hodari kunywa kileo chenye nguvu, watu waume wenye nguvu huchanganya vileo, wampao haki mwenye uovu ili wapewe ijara na kumwondolea mwenye haki haki yake.
(Isaya 5;22-23).

Ole wa taji ya kiburi ya walevi wa Efraim na ua la uzuri wa fahari yake linalonyauka, lililo kichwani mwa bonde linalostawi la hao walioshindwa na divai!

(Isaya 28:1).

Uzinzi na divai, na divai mpya huondoa fahamu za wanadamu. (Hosea 4:11).

## Saumu

Akafunga siku arubaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. (Mathayo 4:2).

Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga. (Mathayo 17:21).

## Kutahiriwa

Siku ya nane mtoto atatahiriwa govi la zunga lake. (Mambo ya Walawi 12:3).

Mungu akamwambia Ibrahimu, nawe ulishike agano langu wewe na uzao wako kwa vizazi vyao baada yako. Hili ndilo agano langu utakalolishika, kati ya mimi na wewe na uzao wako baada yako kila mwanamume wa kwenu atatahiriwa. Mtatahiriwa nyama ya magovi yenu na jambo hilo litakuwa ishara ya agano kati ya mimi nanyi. (Mwanzo 17:9-11).

Ibrahim mwenyewe alitahiriwa tena katika umri wa miaka 99. Na Ismail pia alitahiriwa siku hiyo hiyo. (Mwanzo 17:24-27).

Yohana alitahiriwa baada ya siku 8. (Luka 1:59).
Yesu pia alitahiriwa baada ya siku 8. (Luka 2:21).
Paulo mwenyewe alitahiriwa. (Wafilipi 3:5).
Paulo ndiye ambaye alifundisha kinyume cha agano hilo kati ya Mungu na Ibrahimu. (Wagalatia 5:2-6).

## Yesu hakuzaliwa Disemba 25

Hata ikawa katika mwaka wa thelathini na saba wa kuhamishwa kwake Yehoyakini, mfalme wa Yuda, katika mwezi wa kumi na mbili, siku ya ishirini na tano ya mwezi wa Evil - Merodaki mfalme wa Babeli, katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake, akamwinua kichwa chake Yehoyakini mfalme wa Yuda akamtoa gerezai. (Yeremia 52:31).

### Idi pia yapatikana katika Biblia

Mtafanya nini katika siku ya mkutano wa Idi; na katika siku ya karamu ya Bwana? (Hosea 9:5).

### Waanzilishi wa Ukristo ni Paulo na Barnabas.

Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia (Matendo 11:26).

### Harusi ya Kaini.

Kaini akatoka mbele ya uso wa Bwana akakaa katika

nchi ya Nodi mbele ya Adeni. Kaini akamjua mkewe naye akapata mimba akamzaa  Enoko naye akajenga mji akauita Henoko kwa jina la mwanawe.
(Mwanzo 4:16-17)

## Kukumbuka kwa urahisi

1.  Yesu hakufufuka.                (1Wakorintho 15;15).
2. Mwandishi wa Mathayo si Mathayo.     (Mat. 9:9).
3. Wanawake na wanaume wasichanganyike
(Zakaria 12:12).
4. Nabii mfano wa Musa atakuja.     (Kumb. 18:18).
5. Taurati iwe uwongo.                         (Yer. 8:8).
6. Ismail akakaa katika jangwa la Paran na mama yake.
(Mwanzo 21:21).
7.  Naye Ibrahimu alikuwa mtu wa miaka 86, hapo Hajira alipomzalia Ibrahimu Ismail.  (Mwanzo 16:16).
8. Wale wanaomwita Yesu Bwana Bwana na wanatoa mapepo kwa jina lake watafukuzwa siku ya Kiyama.                               (Mat. 7:22-23).
9. Waacheni wafu wazike wafu wenzao. (Mat. 8:22).
10.  (Yesu alisema) Wote walionitangulia ni wevi na wanyang'anyi.                           (Yohana  10:8)
11. Yesu aliwaambia amani iwe kwenu (yaani Assalaamu Alaikum).                 (Yohana 20:19).
12. Yesu alikuwa akienda sinagogi.       (Luka 4:16).
Sinagogi ni msikiti (maelezo ya maneno).
13.  Msimwambie yeyote kwamba mimi ni Kristo.

(Mat:16:20).
14. Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu.
(Mat. 17:20).
15. Sanamu zao ni fedha na dhahabu kazi ya mikono ya wanadamu, zina vinywa lakini hazisemi, zina macho lakini hazioni, zina masikio lakini hazisikii, zina pua lakini hazisikii harufu, zina mikono lakini hazishiki, zina miguu lakini haziendi wala hazitoi sauti kwa koo zake. (Zaburi 115:4-7).
Je, sanamu za Mariamu na Yesu hazipatikani makanisani?

## Maswali Kwa Wakristo

Hapa chini ninaandika baadhi ya maswali kwa ajili kuwauliza akina mapadri na ndugu Wakristo, ili watusaidie majibu sawa na Bibilia.
1. Katika aya gani ya Biblia Mwenyezi Mungu amesema kwamba Yesu ni Mungu?
Katika aya gani ya Injili Bwana Yesu amedai kuwa 2. yeye ni Mungu?
Kama Yesu ni Mwana wa Mungu, basi Mungu na 3. Mariamu (Mama wa Yesu), wanao uhusiano gani baina yao. Maana Mungu hawezi kupata mtoto bila ya mke, basi mke wa Mungu ni nani?
"Inamkinikaje awe na mwana hali hana mke (Qur'an 6:102).
Biblia inasema: Akaenda, akakaa katika mji ulioitwa 4.

Nazareti, ili litimie neno lililonenwa na manabii, ataitwa Mnazarayo. (Mat: 2:23).
Hawa manabii ni akina nani na walinena wapi?.
Ushahidi wa kitabu unahitajika.

Je unakubali kwamba Yesu ni mwizi? Kwa sababu 5.
mwenyewe amesema kwamba ujaji wake wa mara ya pili utakuwa sawa na ujaji wa mwizi. (Mat 24:43; Ufunuo 3:3 na Petro 3:10).

Iwapo unapenda kununua vitabu zaidi vya Dini ya Kiislamu au kwa maelezo zaidi ya mafundisho ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, wasiliana na anuani iliyo karibu nawe kati ya hizi zifuatazo:

P. O. Box 376, Simu: 2110473 Dar es Salaam. 1.
P. O. Box 1, Simu: 2603477 Morogoro. 2.
P. O. Box 260, Simu: 2646849 Tanga. 3.
P. O. Box 359 Iringa. Simu 2700633. 4.
P. O. Box 196, Simu: 243043 Dodoma. 5.
P. O. Box 94, Simu: 2600847 Songea. 6.
P. O. Box 10723 Arusha. 7.
P. O. Box 54, Simu: 2603291 Tabora. 8.
P. O. Box 547 Ujiji - Kigoma. 9.
P. O. Box 306, Simu: 2333919 Mtwara. 10.
P. O. Box 86, Simu: 2510082 - Masasi. 11.
P. O. Box 1812 Bukoba. 12.
P. O. Box 28, Simu 70 Kibiti - Rufiji. 13.
P. O. Box 391 Tarime. 14.
P. O. Box 605 Ifakara. 15.
P. O. Box 17 Kilosa. 16.
P. O. Box 40554, Simu: 764226 Nairobi Kenya. 17.
P. O. Box 97011, Simu: 492624 Mombasa Kenya. 18.
P. O. Box 421, Simu 40269 Kisumu Kenya. 19.
P. O. Box 77, Simu 52 Shianda Kenya. 20.
P. O. Box 552 Limbe Malawi. 21.